

# UJUMBE KUTOKA KWA
## MKURUGENZI WA MISITU NA NYUKI

**Mpendwa Msomaji,**
Napenda kukukaribisha tena kwenye toleo letu la pili la Jarida lako pendwa la *Misitu ni Mali* kwa mwaka wa 2022. Toleo la kwanza lilikuhabarisha kuhusu masuala kadhaa yaliyofanyika katika sekta za misitu na ufugaji nyuki tangu toleo la mwisho la Jarida hili lililotoka mwaka 2018. Toleo lililopita lilibainisha kuandaliwa kwa mikakati ya utekelezaji wa sera za taifa za misitu na ufugaji nyuki, kutungwa na kuboreshwa kwa kanuni mbalimbali za misitu, kuanza kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali inayosimamiwa na Idara, kuidhinishwa kwa miongozo mbalimbali ya usimamizi wa sekta za misitu na ufugaji nyuki, uendelezaji wa jeshi la uhifadhi na taarifa juu ya tathmini ya mchango wa sekta ya misitu katika pato la Taifa.

Toleo hili linakuletea taarifa kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa masuala hayo ikiwemo, masuala mapya yaliyotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2022. Miongoni mwa masuala hayo ni;

- Ushiriki wa Wizara katika Kongamano la Kimataifa la APIMONDIA jijini Instanbul nchini Uturuki Ililofanyika kuanzia Agosti 24 hadi 28 Agosti, 2022
- Ushiriki wa Wizara katika kampeni ya upandaji miti kwenye vyanzo vya maji iliyofanyika jijini Mbeya Novemba 15, 2022 iliyoongozwa na Mhe. Dkt. Isdory Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Uzinduzi wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki - NABAC

Mpendwa msomaji nina imani kupitia jarida hili utapata kufahamu hatua mbalimbali zilizofikiwa katika kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki hapa nchini. Wito wangu kwenu ni kuendelea kuimarisha uhusiano tulioujenga kwa miaka mingi na kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kuhakikisha tunaleta mageuzi chanya katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hizi hapa nchini. Juhudi hizi za kuwaletea habari mbalimbali zitakuwa endelevu ili kuhakikisha sisi sote tunafahamu nini Serikali imepanga na matarajio yake katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki hapa nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

**Nawatakia kila la kheri.**



Bw. Deusdedit K. Bwoyo
**Mkurugenzi, Idara ya Misitu na Nyuki**

# TANZANIA YATANGAZA FURSA ZA UFUGAJI NYUKI KIMATAIFA

*Na: Petro Mholage, FBD*

Kupitia mikutano na maonesho mbalimbali Tanzania imekuwa ikitangaza fursa zilizopo katika sekta ya ufugaji nyuki kwa lengo la kuvutia wawekezaji wakubwa wa ndani na nje kuwekeza kwenye ufugaji nyuki kibiashara, kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao ya nyuki na kutumia makundi ya nyuki kwenye uchavushaji wa mimea. Tanzania imeendelea kutangaza fursa hizo katika matukio mbalimbali kama vile Kongamano la 47 la Ufugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA) lililofanyika Agosti 24 – 28, 2022 nchini Uturuki. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mkurugenzi msaidizi wa Idara ya Misitu na Nyuki Bw. Daniel Pancras ulipata nafasi ya kuonesha bidhaa zitokanazo na nyuki zinazozalishwa nchini, kufanya mikutano na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki kwa lengo la kuwashawishi kufanya biashara na makampuni yaliyopo nchini yanayofanya biashara ya mazao ya nyuki. Vilevile, ujumbe umekutana na wenye viwanda vya kuongeza thamani mazao ya nyuki na watengenezaji wa vifaa mbalimbali vya kufugia na kuchakata mazao ya nyuki kwa lengo la kuwashawishi kuja kuwekeza nchini.




Akiongea na *Misitu ni Mali* Mkurugenzi Daniel alisema, wafanyabiashara kutoka nchi za Uturuki, Saudi Arabia, Canada, Uingereza, Marekani, Brazil na Morocco wameonesha nia ya kufanya biashara na wasambazaji na wasafirishaji wa mazao ya nyuki wa Tanzania.

Baadhi ya mambo ambayo ujumbe wa Tanzania ulitekeleza ni pamoja na kuwashawishi wenye viwanda vya kuongeza thamani mazao ya nyuki kuja kuwekeza nchini kwa kujenga viwanda vya kutengeneza vipodozi na vile vya kutengeneza dawa mbalimbali zinazotumia mazao ya nyuki na kuanzisha kituo cha tiba (*Api-therapy*) kitakachotumia mazao ya nyuki kama vile sumu ya nyuki.

Kwa upande mwingine timu ya Tanzania ilifanya kikao na Rais wa APIMONDIA Kamisheni ya Afrika, Bw. David Mukomana, kwa lengo la kueleza nia ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Kongresi ya 50 ya APIMONDIA inayotarajiwa kufanyika katika moja ya nchi wanachama kutoka Afrika mwaka 2027. Kupitia kikao hicho kiongozi wa Kamisheni alieleza kuwa Tanzania ni moja ya nchi zilizo katika Bara la Afrika yenye nafasi kubwa ya kushinda nafasi ya kuwa mwenyeji wa kongamano hili ifikapo mwaka 2027.

Bwana David aliueleza kuwa "kwa vile Tanzania ina eneo kubwa la misitu linalofaa kwa ufugaji nyuki, hali hiyo inaipa Tanzania uwezekano wa kufikiriwa kuandaa APIMONDIA 50.

Iwapo Tanzania itaandaa Kongamano la APIMONDIA 50 itakuwa ni fursa kwa wadau wengi wa ufugaji nyuki kuja kujifunza mambo mbalimbali.

Tanzania ni nchi pekee inayotambua ufugaji nyuki kama sekta rasmi inayochangia katika uchumi wa kaya na Taifa kwa ujumla.

Kupitia kongamano hilo Tanzania imetangaza fursa za ufugaji nyuki zilizopo nchini, hivyo kuwepo kwa uwezekano mkubwa kwa wawekezaji wa nje kuvutiwa na kuja kushiriki katika kuendeleza sekta hii. Vilevile, kongamano hilo limeunganisha wafugaji nyuki na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki wa ndani na wale wa nje ya nchi kwa lengo la kuanza kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya ufugaji nyuki.

Aidha, kushiriki kongamano hilo kumechochea ufugaji nyuki kibiashara hivyo kutaongeza ajira na pato la kaya na Taifa kwa ujumla. Pia, kongamano limeimarisha mtandao wa masoko ya mazao ya nyuki; ushirikiano na nchi wanachama wa APIMONDIA katika maeneo mbalimbali ya sekta ya ufugaji nyuki; na kuchochea shughuli za utalii kwa kushawishi washiriki kutembelea vivutio vya utalii ikizingatiwa kongamano hilo limehudhuriwa na washiriki kutoka takriban nchi 150. Tanzania kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na sekta binafsi inaendelea na maandalizi yatakayowezesha kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa kongamano hilo la APIMONDIA ya 50.




Tanzania ni moja ya nchi za Afrika zenye fursa kubwa ya uzalishaji na uchakataji wa mazao ya nyuki. Tanzania ina eneo linalokadiriwa kuwa na hekta takribani milioni 48.1 za misitu ambazo kwa ujumla zinafaa kwa shughuli za ufugaji nyuki. Aidha, asilimia 93 ya eneo hilo la misitu ni misitu ya mataji wazi (woodlands) ambayo imesheheni mimea yenye maua yanayofaa kwa ajili ya ufugaji nyuki. Uwepo wa misitu ya miombo, vichaka vya Itigi, na mikoko unaifanya Tanzania kuzalisha asali bora na yenye soko ndani na nje ya nchi. Kwa sasa, Tanzania ni nchi ya 14 duniani na ya pili Afrika kwa uzalishaji wa asali. Katika jitihada za kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki, Serikali na Sekta Binafsi kwa pamoja wameweka mikakati itakayowezesha Tanzania kuwa katika nchi kumi bora duniani na ya kwanza Afrika kuzalisha asali na nta zenye ubora. Miongoni mwa mikakati iliyopo ni kuhamasisha wafugaji nyuki kufuga kibiashara. Hii inafanyika kwa kuanzisha mashamba makubwa ya nyuki na kuwekeza katika viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani mazao ya nyuki.

# MAKAMU WA RAIS AIAGIZA TFS KUZALISHA MICHE RAFIKI YA VYANZO VYA MAJI

*Na: Kassim Ally, TFS*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango ameuagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kutambua miti rafiki ya maji na kuandaa miche ya miti hiyo kwa lengo la kuipanda kwenye vyanzo vya maji. Mhe. Dkt. Mpango aliyasema hayo Novemba 16, 2022 wakati akizindua Kampeni ya kitaifa ya upandaji miti rafiki kwenye vyanzo vya maji. Pia, TFS imetakiwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya miti rafiki ya maji ili kunusuru vyanzo vya maji. Kampeni hiyo ilizinduliwa katika chanzo cha maji cha Nzovwe Kata ya Mwakibete Jijini Mbeya kwa Makamu wa Rais kupanda mti. Aidha, Mhe. Dkt. Mpango alizitaka mamlaka husika kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya gesi ya kupikia ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambavyo huchangia uharibifu wa mazingira. Vilevile, Mhe. Makamu wa Rais amewaagiza Wakuu wa Mikoa nchini kuzindua kampeni ya upandaji miti rafiki ya maji katika maeneo yao ili kufikia lengo la mwaka huu kupanda miti milioni 2.5.

Wakati huohuo katika Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Kitaifa ya Kupanda Miti yaliyofanyika Wilayani Magu Machi 21, 2022 Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii Mhe. CPA Mary Masanja (Mb) aliiagiza TFS na Mfuko wa Misitu Tanzania - (TaFF) kushirikiana kwa kuanzisha kitalu cha miche ya miti Wilayani hapo.

Katika kutekeleza agizo hilo kuanzia Juni 2022, TFS na TaFF zilianzisha kitalu cha miche ya miti katika ofisi za misitu za Wilaya ya Magu. Kwa kuanzia kitalu hicho kina zaidi ya miche 120,000 ya miti ya aina mbalimbali ikiwemo miche ya miti ya Mkaratusi; Mkangazi, Mwerezi, Mwarobaini na Mhale/Mgunga, na miti ya matunda kama Miembe, Mchungwa, Mchenza, na Mlimao. Lengo la kitalu hicho ni kuotesha miche ya miti ya matumizi mbalimbali 300,000 ifikapo Machi 2023. Miche itakayozalishwa kwenye kitalu hiki itasambazwa kwa wananchi wa Wilaya ya Magu na maeneo mengine ya Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa.

Katika kufuatilia agizo hilo Agosti 21, 2022 Mhe. CPA Mary Masanja (Mb) alifanya ziara Wilayani Magu kwa lengo la kukagua maendeleo ya kitalu hicho cha miche ya miti.

Katika maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Kitaifa ya Kupanda Miti mwaka 2022, TFS ilitoa miche ya miti kwa baadhi ya wananchi waliohudhuria maadhimisho hayo. Upatikanaji huo wa miche ya miti umehamasisha wananchi wa Wilaya ya Magu na Kanda ya Ziwa kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika kupanda miti. Aidha, umma ulielimishwa juu ya umuhimu wa uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na upandaji miti. Mbali na kuanzisha kitalu hicho cha miche ya miti, TFS na Kituo cha Afya Sengerema walipanda miti na kukagua maendeleo ya miti ya mijohoro iliyopandwa katika eneo la kituo hicho. Pia TFS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita ilianzisha Kampeni ya Upandaji Miti katika maeneo ya mji huo. Kampeni hiyo ilizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita kwa kupanda miti kwenye barabara za mji wa Geita zenye urefu wa zaidi ya kilometa 1.5.

Katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanajenga tabia ya kupanda miti matukio mengi ya kitaifa yamekuwa yakijumuisha zoezi la upandaji miti. Mfano, katika kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, TFS kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Kanda ya Ziwa imepanda miti idadi ikiwa kwenye mabano. Ukerewe (1,500), Sengerema (4,560), Nyang'wale (4,200), Bunda (800), Bukombe (100,000), Misungwi (2,000), Misenyi (624), Kyerwa (1,298), na Mbogwe (300).

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
MFUKO WA MISITU TANZANIA

Kwa Kudumisha Ugharimiaji
wa Usimamizi wa Misitu

# UTARATIBU WA KUOMBA RUZUKU INAYOTOLEWA NA MFUKO WA MISITU TANZANIA

## 1.0 UTANGULIZI

Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) umeanzishwa chini ya Sheria ya Misitu Sura 323 kwa lengo la kuwa chanzo endelevu cha fedha kwa ajili ya kuwezesha uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu hapa nchini. Mfuko huu upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na unasimamiwa na Bodi ya Wadhamini. Mfuko wa Misitu Tanzania ulianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Julai 2011.

Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa uwezeshaji wa miradi kupitia utoaji ruzuku. Aidha, utoaji wa ruzuku unaongozwa na Kanuni zinazojulikana kwa lugha ya kiingereza kama ***"The Forest (Manner and Criteria for Awarding Grants) Regulations, 2021"***. Kwa mujibu wa Kanuni hizo zinazoongoza utoaji ruzuku za mwaka 2021, ruzuku inatolewa baada ya kuwasilishwa kwa maombi kwa kuzingatia vipaumbele vya mwaka husika na maombi hayo kukidhi vigezo vya kupatiwa ruzuku. Aidha, Tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku hutolewa mwezi **Desemba kila mwaka** na mwisho wa kupokea maombi ya ruzuku ndogo, ruzuku ya kati na ruzuku kubwa ni tarehe **31 Machi kila mwaka**.

## 2.0 WALENGWA (WANAOWEZA KUOMBA RUZUKU)

Kwa mujibu wa Kanuni zinazoongoza utoaji ruzuku za mwaka 2021, walengwa wanaoweza kuomba ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania wamegawanyika katika makundi yafuatayo:

i) Watu binafsi;
ii) Vikundi vya kijamii (CBOs);
iii) Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs);
iv) Asasi za kiraia (CSOs),
v) Jumuiya/taasisi za kidini (FBOs);
vi) Taasisi za mafunzo;
vii) Taasisi za utafiti; na
viii) Taasisi za Serikali (shule za msingi na sekondari, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali).

### 2.1 Watu Binafsi

Watu binafsi wanaruhusiwa kuomba ruzuku ndogo ya kiasi cha fedha kisichozidi **shilingi Milioni Tano (5,000,000/=)**. Aidha, watawasilisha andiko la kuomba ruzuku lililoandaliwa kwa kufuata muundo utakaooneshwa katika Tangazo la kuitisha maandiko la mwaka husika.

### 2.2 Vikundi vya kijamii (CBOs)

Vikundi vya kijamii vinaruhusiwa kuomba ruzuku ndogo ya kiasi cha fedha hadi **shilingi Milioni Kumi (10,000,000/=)**. Aidha, vikundi vitawasilisha maandiko ya kuomba ruzuku yaliyoandaliwa kwa kufuata muundo utakaooneshwa katika Tangazo la kuitisha maandiko la mwaka husika:

### 2.3 Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), Asasi za kiraia (CSOs) na Jumuiya/mashirika ya dini (FBOs)

Mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia na jumuiya/ mashirika ya dini zinaweza kuomba ruzuku ya kati na ruzuku kubwa (kama zilivyofafanuliwa katika kipengele namba 4). Aidha, NGOs, CSOs na FBOs zitawasilisha maandiko ya kuomba ruzuku yaliyoandaliwa kwa kufuata muundo utakaooneshwa katika Tangazo la kuitisha maandiko la mwaka husika:

### 2.4 Taasisi za mafunzo na Taasisi za utafiti

Taasisi za mafunzo na Taasisi za utafiti zinaweza kuomba aina zote za ruzuku isipokuwa ruzuku ndogo ambayo ni kwa ajili ya watu binafsi na vikundi vya kijamii na ruzuku maalum ambayo ni kwa ajili ya taasisi za serikali tu (zikiwemo taasisi za mafunzo na taasisi za utafiti za Serikali). Waombaji wa kundi hili watawasilisha maandiko ya kuomba ruzuku yaliyoandaliwa kwa kufuata muundo utakaooneshwa katika Tangazo la kuitisha maandiko la mwaka husika:

### 2.5 Taasisi za Serikali

Taasisi za Serikali zinaweza kuomba ruzuku ya kati, ruzuku kubwa na ruzuku maalum. Aidha, kwa ruzuku maalum anayeruhusiwa kuomba ni Mkuu wa Taasisi tu. Waombaji wa kundi hili watawasilisha maandiko ya kuomba ruzuku yaliyoandaliwa kwa kufuata muundo utakaoainishwa katika Tangazo la kuitisha maandiko la mwaka husika:

### 2.6 Vielelezo vinavyohitajika wakati kuwasilisha maombi ya kuomba ruzuku

Walengwa wa ruzuku wanashauriwa kabla ya kuwasilisha maombi wazingatie kuwa wametimiza masharti ya vielelezo vinavyohitajika kuambatishwa pamoja na andiko. Vielelezo hivyo ni kama ifuatavyo:

i) Barua ya udhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata anapoishi mwombaji wa ruzuku (kwa walengwa wote isipokuwa Taasisi za Serikali na wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu);

ii) Barua ya udhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji mradi utakapotekelezwa (kwa walengwa wote isipokuwa Taasisi za Serikali na wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu);
iii) Barua ya udhamini kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri mradi utakapotekelezwa (kwa walengwa wote isipokuwa Taasisi za Serikali na wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu);
iv) Muhtasari wa kikao cha familia kinachoonesha jinsi mradi unaoombewa ruzuku utakavyotekelezwa iwapo mwombaji wa ruzuku atafikwa na umauti (kwa muombaji ambaye ni Mtu binafsi);
v) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (kwa muombaji binafsi);
vi) Uthibitisho wa umiliki wa ardhi (barua, hati miliki, hati miliki za kimila, mkataba au hati ya mauziano ya ardhi, barua kutoka mamlaka husika), kwa miradi ya upandaji miti;
vii) Kibali cha kuruhusiwa kufanya shughuli za ufugaji nyuki ndani ya misitu ya hifadhi au maeneo mengine yaliyohifadhiwa (kwa miradi ya ufugaji nyuki);
viii) Uthibitisho wa kudahili wa kutoka Chuo husika kwa wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu;
ix) Barua kutoka Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia utawala ya kuthibitisha kuwa mwombaji wa ruzuku kwa ajili ya kugharamia utafiti ili kukamilisha shahada ya uzamili au uzamivu hana chanzo kingine cha fedha kwa ajili ya kugharamia utafiti huo;
x) Barua ya utambulisho na barua ya udhamini kutoka kwa Mkuu wa Idara alipodahiliwa mwanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu.
xi) Barua ya utambulisho na udhamini kutoka Mkuu wa Taasisi iwapo mwombaji ni Idara au Kituo;
xii) Uthibitisho wa uwepo wa ofisi ya NGOs, CSOs au FBOs (barua kutoka kwa mamlaka husika);
xiii) Barua ya udhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata ilipo ofisi ya NGOs, CSOs au FBOs;
xiv) Barua ya udhamini kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji mradi utakapotekelezwa (kwa walengwa wote isipokuwa Taasisi za Serikali na wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu);
xv) Barua ya udhamini kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri mradi utakapotekelezwa kwa walengwa wote isipokuwa Taasisi za Serikali na wanafunzi wa shahada ya uzamili au uzamivu);
xvi) Kivuli cha cheti cha usajili wa ofisi ya NGOs, CSOs au FBOs;
xvii) Barua ya kuthibitisha kuwa NGOs, CSOs au FBOs imehakikiwa na mamlaka husika;
xviii) Kivuli cha cheti cha usajili wa kikundi kilichothibitishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kiliposajiliwa kikundi;
xix) Muhtasari wa kikao cha wanachama kilichopitisha andiko la mradi wenu. Aidha, muhtasari usainiwe na wanachama wote (Vikundi, NGOs, CSOs au FBOs)
xx) Kibali cha kuruhusiwa kufanya shughuli za ufugaji nyuki ndani ya misitu ya hifadhi au maeneo mengine yaliyohifadhiwa (kwa miradi ya ufugaji nyuki).
xxi) Barua ya utambulisho na udhamini kutoka kwa Mkuu wa Taasisi iwapo mwombaji ni Idara au Kituo (kwa Taasisi za Mafunzo, Utafiti na Taasisi za Serikali);

## 3.0 MAENEO YA KIPAUMBELE YATAKAYOZINGATIWA KATIKA UTOAJI WA RUZUKU

Katika utoaji wa ruzuku, Mfuko wa Misitu Tanzania utazingatia vipaumbele vifuatavyo:

**3.1** Uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Aidha, ***Kila mwaka Mfuko utaainisha shughuli zitakazogharamiwa na mikoa itakayopewa kipaumbele.***

**3.2** Uboreshaji wa maisha ya jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu ya hifadhi, hususani miradi inayohusiana na ufugaji nyuki inayolenga kuboresha uhifadhi wa misitu. Aidha, ***Kila mwaka Mfuko utaainisha shughuli zitakazogharamiwa na mikoa itakayopewa kipaumbele.***

**3.3** Utafiti wa Misitu unaolenga kuboresha uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu na kuongezea thamani mazao ya misitu na nyuki. Miradi ya utafiti itakayofikiriwa kupatiwa ruzuku inapaswa kutokana na maeneo ya utafiti yaliyopo kwenye **Mpango Kabambe wa Taifa wa Utafiti wa Misitu** (***National Forest Research Master Plan III) na*** **Mpango Kabambe wa Taifa wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki** (***National Beekeeping Research Master Plan I).*** Walengwa katika kipaumbele cha miradi ya utafiti ni Taasisi za Utafiti, Taasisi za Mafunzo na watafiti kutoka Taasisi za Utafiti na Taasisi za Mafunzo, na miradi ya utafiti inaweza kutekelezwa sehemu yeyote katika mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku la kila mwaka litatoa ufafanuzi zaidi.

### 3.4 Kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali za Mafunzo na Utafiti

Maandiko ya miradi ya kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali za Mafunzo na Utafiti za sekta ya misitu zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii yatakayofikiriwa kupatiwa ruzuku. Lengo ni kujenga uwezo wa kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa majukumu yenye mchango chanya katika kuboresha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu kwa maendeleo endelevu.

## 4.0 AINA ZA RUZUKU ZINAZOTOLEWA NA MFUKO WA MISITU TANZANIA

Kwa mujibu wa Kanuni za kuongoza utoaji ruzuku za mwaka 2021, Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa aina nne za ruzuku ambazo ni:

**4.1 Ruzuku Ndogo ambayo imegawanyika katika makundi mawili:**

i) Kiasi cha fedha kisichozidi Shilingi Milioni Tano (5) ambayo hutolewa kwa watu binafsi na shule za msingi na sekondari.

ii) Kiasi cha fedha kinachozidi Shilingi Milioni Tano (5) lakini hakizidi Shilingi Milioni 10. Walengwa wa ruzuku ya kundi hili ni vikundi vya kijamii vinavyotekeleza miradi ya upandaji miti au ufugaji nyuki, lakini makundi mengine yanaweza kuomba ruzuku ndogo ya kundi hili isipokuwa watu binafsi.

***Ruzuku ndogo ni kwa ajili ya miradi ambayo utekelezaji wake hauzidi mwaka mmoja.***

**4.2 Ruzuku ya Kati:** kiasi cha fedha kinachozidi **Shilingi Milioni 10** lakini hakizidi **Shilingi Milioni 20**. Ruzuku hii hutolewa kwa walengwa (wanaoweza kuomba ruzuku) waliotajwa katika kipengele namba mbili (2) isipokuwa watu binafsi na vikundi vya kijamii. ***Ruzuku ya kati ni kwa ajili ya miradi ambayo utekelezaji wake unazidi mwaka mmoja na unaweza kuchukua hadi miezi 18***.

**4.3 Ruzuku Kubwa:** kiasi cha fedha kinachozidi **Shilingi Milioni 20** lakini hakizidi **Shilingi Milioni 50**. Ruzuku hii hutolewa kwa walengwa (wanaoweza kuomba ruzuku) waliotajwa katika kipengele namba mbili (2) isipokuwa watu binafsi na vikundi vya kijamii. ***Ruzuku kubwa ni kwa ajili ya miradi ambayo utekelezaji wake unazidi mwaka mmoja na unaweza kuchukua hadi miaka miwili***.

**4.4 Ruzuku Maalum:** Kiasi cha fedha kinachozidi **Shilingi Milioni 50**. Walengwa wa ruzuku ya kundi hili ni **Taasisi za Serikali tu** na maandiko ya kuomba ruzuku yanaweza kuwasilishwa wakati wowote. Ruzuku maalum ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ambayo itatoa mchango mkubwa katika uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Aidha, tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku la kila mwaka litatoa ufafanuzi zaidi kuhusu aina ya miradi itakayopatiwa ruzuku kwa mwaka husika.

## 5.0 KUANDAA MAANDIKO KWA AJILI YA KUOMBA RUZUKU

Maandiko ya kuomba ruzuku yanapaswa kuandaliwa kwa kutumia miundo itakayooneshwa kwenye tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku la kila mwaka. Tangazo hilo litatolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo magazeti, mitandao ya kijamii (twitter, instagram, facebook na yuotube), kupitia tovuti ya Mfuko wa Misitu Tanzania ambayo ni www.mfukowamisitu.go.tz na tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii www.maliasili.go.tz na tovuti za taasisi nyingine zinazojihusisha na uhifadhi. Aidha, Tangazo litapatikana katika ofisi za taasisi mbalimbali zikiwemo ofisi za Kanda na Wilaya za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Ofisi za Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs).

## 6.0 UWASILISHAJI WA MAANDIKO YA KUOMBA RUZUKU

Waombaji wa ruzuku wanapaswa kuwasilisha maandiko ya kuomba ruzuku kupitia njia zifuatazo:

**6.1 Kutumia Mfumo / Mtandao *(Online Application)***
Watakaoomba ruzuku kwa njia ya mtandao *(online application)* wataingia katika mfumo kwa kutumia anwani *(link)* ifuatayo: au **https://portal.maliasili.go.tz/** na kufuata maelekezo yaliyopo. Aidha, tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku la kila mwaka litaweka namba ya simu ya wataalam wa TEHAMA ambao watatoa msaada kwa watakaopata changamoto ya kutumia mtandao.

**6.2 Kuwasilisha Maandiko ya Kuomba Ruzuku kwa njia ya Posta**
Waombaji wa ruzuku ambao hawana uwezo wa kuwasilisha maandiko ya kuomba ruzuku kwa kutumia mtandao (hasa vikundi), wanaweza kuomba kibali cha kuwasilisha nakala za kine *(hard copies)* kwa Katibu Tawala wa Mfuko wa Misitu Tanzania kupitia anwani ya Posta hapo chini.

Aidha, waombaji waliopatiwa kibali cha kuwasilisha nakala za kine *(hard copies),* wanaweza kuwasilisha maandiko yao moja kwa moja kwenye ofisi za Mfuko wa Misitu Tanzania zilizopo ghorofa ya kwanza katika Jengo la Bodi ya Mfuko wa Barabara, Eneo la Uwekezaji Njedengwa karibu na Jengo la Tume ya Uchaguzi.

***ANGALIZO: Maombi ya ruzuku yatakayowasilishwa kwa njia ya baruapepe hayatapokelewa. Waombaji wenye uwezo wa kutumia baruapepe wanashauriwa kutumia mfumo wa kielekitroniki kuwasilisha maombi yao.***

## 7.0 VIGEZO VINAVYOTUMIKA WAKATI WA KUCHAGUA MIRADI ITAKAYOPATIWA RUZUKU

Vigezo vitakavyotumika wakati wa kuchagua miradi itakayopatiwa ruzuku vitaainishwa katika tangazo la kuitisha maandiko ya kuomba ruzuku la mwaka husika.

***Kwa watakaotaka kuomba kibali cha kuwasilisha maombi ya ruzuku kwa njia ya posta na watakaohitaji maelezo ya ziada wanaombwa kuwasiliana na Mfuko wa Misitu Tanzania kupitia anuani ifuatayo:***

*Katibu Tawala,*
*Mfuko wa Misitu Tanzania,*
*Jengo la Bodi ya Mfuko wa Barabara,*
*Ghorofa ya Kwanza,*
*S.L.P. 1764,*
***DODOMA.***

*Simu: +255 (0)26 2963290*
*Nukushi: +255 (0) 2963291*
*Baruapepe: barua@mfukowamisitu.go.tz*
*Tovuti: www.mfukowamisitu.go.tz*

Imeandaliwa na Stephen Msemo Afisa Miradi - TaFF

# WAZIRI PINDI CHANA AITAKA NABAC KUSHAURI NAMNA YA KUENDELEZA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI

*Na: Veneranda Mnyambii, FBD*

Waziri wa Malisili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), ameilekeza Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC) kuishauri Serikali namna bora ya upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kufugia nyuki, uchakataji na ufungashaji mazao ya nyuki kwa gharama nafuu. "Ni jukumu lenu kuishauri serikali namna gani inaweza kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki angalau kufikia asilimia 50 ya uwezo uliopo," alisisitiza Mhe. Dkt. Chana na kuongeza. "Aidha, Serikali inawategemea kuishauri kuhusu utaratibu utakaoimarisha ushirikiano baina yake na wadau wa sekta ya ufugaji nyuki mfano watu binafsi, vikundi na hata vyama vya ushirika ili kuleta ufanisi na tija." Mhe. Balozi Dkt. Chana aliyasema hayo wakati anazindua Kamati hiyo Jijini Dodoma Septemba 21, 2022.



*Waliokaa katikati ni Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii (Mb), kulia kwake ni Bw. Juma Mkomi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, kushoto kwake ni Bw. Deusdedit Bwoyo, Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki. Waliosimama ni wajumbe wa NABAC*

Mhe. Dkt. Chana alielekeza Kamati ishauri namna bora ya kukabiliana na uharibifu wa maeneo yenye rasilimali za ufugaji nyuki na namna bora ya kuimarisha Utalii wa Nyuki kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta inachangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa utalii hapa nchini. "Mbali na hayo mnatakiwa mje na njia bora ya kutoa mafunzo kwa wadau ili kuwajengea uelewa na mbinu bora za ufugaji nyuki, masuala ya masoko na vifungashio hatimaye sekta iongeze mchango wake katika Pato la Taifa." Alielekeza Mhe. Dkt. Chana.

Aidha, Mhe. Waziri aliielekeza Idara ya Misitu na Nyuki kuandaa Mpango wa kutoa mafunzo yanayohusu mbinu bora za ufugaji nyuki kwa jamii hasa vikundi vya vijana na wanawake. Idara iandae rasimu ya Hati ya Makubaliano (MoU) itakayotumika baina ya taasisi zinazosimamia maeneo ya kufugia nyuki na wafugaji nyuki. Makubaliano hayo yaweke bayana taratibu za kutumia maeneo hayo na kuhakikisha yanahifadhiwa.

Idara pia imetakiwa iandae daftari lenye takwimu zinazoonesha uwepo wa vikundi vya ufugaji nyuki vya vijana na wanawake ambavyo vimeomba kuwezeshwa kupitia asilimia kumi (10%) ya mapato yanayotolewa na kila Halmashauri. Daftari hilo libainishe vikundi vilivyowezeshwa na ambavyo havijawezeshwa ili Wizara iangalie namna ya kuviwezesha pamoja na kuvipa mafunzo.

Idara pia iliagizwa kufanya tathmini ya shughuli za maendeleo ya ufugaji nyuki zinazofanywa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kubaini Halmashauri moja ya mfano itakayotumika kuhamasisha wadau wengine wa sekta hiyo. Waziri aliwahakikisha wajumbe wa kamati kuwa Wizara na taasisi zake itahakikisha kuwa inaweka mpango madhubuti wa namna ya kuwapatia wafugaji nyuki maeneo mbadala ya kufugia nyuki ili kupunguza migogoro.

Nyuki ana faida nyingi kwa maisha ya binadamu na mfumo mzima wa kiikolojia. Miongoni mwa faida hizo ni kuwezesha upatikanaji wa chakula kupitia uchavushaji mazao ya kilimo na mimea mingine, uzalishaji wa mazao ya nyuki kama asali, nta, gundi, sumu ya nyuki na chavua ambavyo pia hutumika kama chakula na malighafi za kutengenezea bidhaa mbalimbali. Nyuki pia huchangia katika upatikanaji wa ajira na kuimarisha afya ya mfumo wa ikolojia.

Katika kuhakikisha kuwa sekta ya nyuki inasimamiwa barabara, Wizara imetoa miongozo na kuwezesha miradi kadhaa kwa lengo la kuihamasisha jamii kushiriki katika ufugaji nyuki kwa ajili ya kujiongezea kipato na kutunza mazingira.

Kamati hiyo ya NABAC ina wajumbe kumi na moja kutoka Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali na itahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 22, 2022 hadi Juni 21, 2025.



# MCHANGO WA TAF KATIKA MAENDELEO YA MISITU

*Na: Heriberth Haule, TAF*

Chama wa Wataalamu wa Misitu Tanzania - TAF kiliundwa rasmi Julai 27, 1976 chini ya Sheria ya Jamii ya mwaka 1954 na kupewa namba ya usajili SO 5979. TAF ni Shirika lisilo la Kiserikali - (NGO) ambalo limeanzishwa kwa ajili ya kufanya shughuli ambazo sio za kibiashara. Chama hiki cha kitaaluma ni moja ya eneo ambalo washauri wa kitaalamu katika masuala ya usimamizi, utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa sekta ya misitu nchini Tanzania hukutana.

**Dira** ya TAF ni kuwa Asasi bora ya kiraia miongoni mwa mashirika yanayotoa huduma ya kitaalamu na ushauri katika sekta ya misitu. Aidha, **Dhamira** ya Chama ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau juu ya usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu nchini ili kuhakikisha rasilimali za misitu zinaongeza mchango wake katika uhifadhi wa mazingira na pato la Taifa.

TAF imeanzishwa kwa ajili ya: kuhamasisha jamii ili ielewe umuhimu wa misitu na utunzaji wa mazingira; kutoa ushauri katika mambo mbalimbali ya sekta ya misitu; kushirikiana na jamii katika shughuli mbalimbali za kupanda na kutunza miti na kupaza sauti mara inapotokea vitendo vinavyoharibu misitu na mazingira. Malengo mengine ni: kuandaa makongamano kwa ajili ya kujadili mambo yahusuyo misitu na utunzaji wa mazingira; kudumisha weledi katika sekta ya misitu; kukusanya taarifa zinazohusu misitu na kuzisambaza; na kuhamasisha utawala bora katika sekta ya misitu. Aidha, TAF inatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, TAF inafanya shughuli zake kupitia kanda zake 11 ambapo mikoa yake imeoneshwa kwenye mabano: Kanda ya Tanga (Tanga), Kanda ya Mashariki (Dar es salaam na Pwani), Kanda ya Morogoro (Morogoro), Kanda ya Ziwa (Kagera, Mwanza, Geita, Simiyu na Mara), Kanda ya Magharibi (Shinyanga, Kigoma na Katavi), Kanda ya Kusini (Lindi na Mtwara), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Ruvuma na Rukwa), Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Manyara) na Kanda ya Zanzibar (Unguja na Pemba), Kanda ya Kati (Dodoma, Singida na Manyara) na Kanda ya Tabora (Tabora).

Katika kipindi cha miaka mitano, TAF imefanya shughuli zifuatazo katika kanda zake. Kazi hizo ni pamoja na: kuelimisha jamii kuhusu njia bora za upandaji miti katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hususan mikoa ya Iringa na Njombe kwa kushirikiana na Programu ya Panda Miti Kibiashara.

Vilevile Chama kilianzisha na kusimamia bustani ya miche ya miti ambayo inafaa kupandwa katika vyanzo vya maji vilivyopo Milima ya Uluguru kwa lengo la kuzuia mmomonyoko wa udongo. Kazi hii ilifanyika kwa ushirikiano na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki - EAMCEF.

Aidha, TAF ilitoa mafunzo ya namna bora ya kupanda miti na kugawa miche 24,000 ya miti kwa jamii zinazozunguka milima ya Uluguru, shule za msingi na sekondari katika Manispaa ya Morogoro, mashirika ya Dini na watu binafsi.

TAF pia iliwawezesha wafugaji nyuki kwa kuwagawia mizinga 20 ya nyuki katika vijiji vya Manza na Mangae vilivyopo Wilaya ya Mvomero. Kazi hii ilitekelezwa kwa kutumia ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania - (TaFF).

Mbali na hayo, Chama kiliandaa Kongamano la Mwaka - (AGM) la wataalam wa misitu ambalo lilihudhuriwa na wadau 300. Kauli mbiu ya kongamano hilo ilikuwa ***Panda miti kwa ajili ya kutunza mazingira na kupunguza***

***umaskini***. Mijadala ya kongamano ilijikita katika mafanikio na changamoto za usimamizi wa misitu kwa lengo la kuboresha hali ya misitu nchini na uhifadhi wa mazingira. TAF pia iliandaa Kongamano la Taifa la uendelezaji wa viwanda vya misitu na nyuki lenye kauli mbiu ***Misitu kwa ajili ya viwanda na maendeleo endelevu***. Katika jitihada za kuitikia wito wa Serikali wa kushirikiana na jamii katika uhifadhi wa misitu, TAF Zanzibar imefanikiwa: kuimarisha uhusiano baina yake na Idara ya Misitu Zanzibar kwa kushirikisha watalaam wa misitu katika kazi za kimaendeleo ya sekta ya misitu na utafiti. Aidha, Chama kilishiriki katika mikutano na vikao mbalimbali.

TAF Zanzibar pia ilishiriki katika shughuli za uhifadhi wa msitu wa asili wa Kiwengwa wenye eneo la hekta 4,333. Huu ni msitu pekee wa asili katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Msitu huo umekuwa ni moja ya vivutio vya watalii na hifadhi kuu ya maji.

TAF imetoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa walimu, wanafunzi na wanajamii wanaozunguka misitu ya Kiwengwa na Masingini kwa kushirikiana na shirika la SEACOLOGY la Marekani. Elimu juu ya ubunifu wa miradi mbalimbali ikiwemo ya ufugaji nyuki na utalii pamoja na utengenezaji wa sabuni zilizonakshiwa kwa viungo ilitolewa. Vilevile, TAF imetoa mizinga, vifaa vya kinga dhidi ya nyuki na vifaa vya kurinia asali.

TAF imewezesha ujenzi wa ofisi ya uhifadhi katika kijiji cha Mwanza (Zanzibar) kwa matumizi ya jamii. Chama pia kimeweka mabango yenye ujumbe wa kuzuia uhalifu katika misitu ya Kiwengwa na Masingini kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa misitu. Chama kimewezesha upandaji miti ya mikoko katika ghuba ya Bumbwini na vyanzo vya maji katika msitu wa asili wa Masingini.

Chama kimefanikiwa kujenga ofisi yake kwenye viwanja vyake vilivyopo katika eneo la Mkundi, barabara ya kwenda Dodoma Manispaa ya Morogoro. Jengo hilo limejengwa kwa nguvu za wanachama. Uzinduzi wa jengo hilo ambalo ni Ofisi ya Makao Makuu ya TAF ulifanyika Desemba 10, 2020, wakati wa kongamano la 19 la Kisayansi lenye kauli mbiu ya ***Misitu kwa Maendeleo Endelevu na Viwanda*** lililofanyika Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) yaliyopo mjini Morogoro. Mkutano Mkuu wa 27 wa Mwaka ulifanyika katika viwanja vya ofisi hiyo ambapo uchaguzi wa viongozi wa sasa ulifanyika.

TAF inatoa wito kwa watalaam wa misitu na nyuki wasio wanachama wajiunge kwa maendeleo ya chama na kubadilishana utaalam na uzoefu.


Kwa mawasiliano zaidi tumia anuani ifuatayo:
Chama cha Wataalam wa Misitu Tanzania - TAF
**“Misitu kwa Maendeleo Endelevu”**
**Plot Na. 507 Y, Eneo la Mkundi,**
**Barabara ya Dodoma,**
**S.L.P 3081, Morogoro, Tanzania**
**Simu: +255 754 448 781**







# UJUE MFUKO WA UHIFADHI WA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (EAMCEF)

EASTERN ARC MOUNTAINS CONSERVATION ENDOWMENT FUND
EAMCEF
MFUKO WA UHIFADHI WA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI

*Na: Francis Sabuni, EAMCEF*

Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ni Mfuko wa Udhamini uliosajiliwa rasmi Juni 2001 chini ya Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini kama ilivyorejelewa mwaka 2002. Mfuko huu ulianzishwa kwa jitihada za pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF), Benki ya Dunia (WB) na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini Waanzilishi. Mfuko huu ni taasisi huru, inayojitegemea na isiyotengeneza faida Mfuko ulianzishwa ikiwa ni mkakati endelevu wa vyanzo vya fedha vya uhakika na vya kudumu kwa ajili ya kuwezesha uhifadhi endelevu wa maliasili zilizomo katika Milima ya Tao la Mashariki nchini, kupunguza umaskini kwa jamii zinazoishi kandokando ya milima hiyo na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Milima ya Tao la Mashariki inaunda ukanda wa milima uliopo Mashariki mwa Afrika ambao unatambuliwa duniani kama moja ya maeneo 34 yenye utajiri mkubwa wa bioanuwai na kwa kuwa na viumbe ndwele wengi wanaokabiliwa na tishio la kutoweka.




*Ramani ya milima ya Tao la Mashariki*

Mfuko unalenga kutoa ufadhili wa muda mrefu na endelevu kwa wanajamii, Idara za Serikali, Halmashauri za Wilaya, mashirika yasiyo ya kiserikali na Taasisi za utafiti ili kutekeleza miradi ya uhifadhi wa maeneo teule, maendeleo ya jamii, mabadiliko ya tabianchi na utafiti wezeshi kwa njia ya uwekezaji au kugharamia moja kwa moja uendeshaji wa miradi husika.

EAMCEF pia inafadhili Hifadhi za Mazingira Asilia za Amani, Kilombero, Nilo, Uzungwa Scarp, Uluguru, Mkingu, Magamba na Chome na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa.

Milima ya Tao la Mashariki ina ukubwa wa takriban kilomita za mraba 5,350. Milima ya Tao la Mashariki inajumuisha Milima ya Upare Kaskazini na Kusini mkoani Kilimanjaro Wilaya za Same na Mwanga, Usambara Magharibi na Mashariki na Nguu ya mkoani Tanga Wilaya za Lushoto, Korogwe, Muheza, Mkinga na Kilindi na Nguru, Uluguru, Ukaguru, Udzungwa, Malundwe, Mahenge na Rubeho ya mkoa wa Morogoro Wilaya za Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kilombero, Ulanga na Manispaa ya Morogoro. Aidha, milima mingine ni Rubeho ya mkoa wa Dodoma Wilaya ya Mpwapwa na Udzungwa mkoa wa Iringa Wilaya za Kilolo na Mufindi. Mfuko huu unasimamiwa na bodi ya wadhamini yenye wajumbe tisa kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii; Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira; Madiwani wawili kutoka maeneo yanayofadhiliwa na Mfuko; sekta binafsi; taasisi za utafiti na vyuo vikuu; jumuiya ya wanasheria, mashirika yasiyo ya kiserikali nchini; na mashirika ya kimataifa. Shughuli za kila siku za uendeshaji wa Mfuko hutekelezwa na Sekretarieti ya Mfuko inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji na Makao Makuu ya Mfuko ni mjini Morogoro.

Manufaa ya kuundwa kwa EAMCEF ni pamoja na: **Kupunguza athari za umaskini:** Bioanuwai ya Milima ya Tao la Mashariki ina manufaa makubwa kijamii katika kupunguza athari za umaskini kupitia mazao ya misitu kama vile kuni, magogo ya kupasua mbao, madawa ya asili, matunda pori na aina nyingine za vyakula ambayo yanakadiriwa kuchangia takriban asilimia 40 ya mahitaji yote ya kaya katika jamii zinazopakana na Milima hiyo.

**Maji:** Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki ni chanzo kikuu cha maji ambacho kwa ujumla hutumika katika viwanda vikubwa nchini pamoja na wananchi wanaokadiriwa kufikia asilimia 25 ya Watanzania wote wanaoishi katika vijiji na miji ya Iringa, Kilolo, Mufindi, Mpwapwa, Morogoro, Kilosa, Gairo, Mvomero, Turiani, Mahenge, Ifakara, Muheza, Chalinze, Korogwe, Lushoto, Mwanga, Same, Soni, Mikumi, Kilindi, Handeni, Kibaha pamoja na majiji ya Dar es Salaam na Tanga.

**Umeme:** Uzalishaji wa umeme nchini unategemea sana ustawi wa misitu ya Milima ya Tao la Mashariki ambayo vyanzo vyake vya maji hutumika kuzalisha zaidi ya asilimia 90 ya umeme wote unaozalishwa nchini katika mabwawa ya Kidatu, Kihansi, Mtera, Pangani, Hale na Nyumba ya Mungu. Aidha, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya umeme wote unaotumika nchini huzalishwa katika mabwawa haya. Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere linalojengwa kwenye maporomoko ya Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) kwa kiasi kikubwa litatumia maji ambayo vyanzo vyake ni Milima ya Tao la Mashariki






*Moja ya kikundi cha ufugaji nyuki kilichopata ufadhili kutoka EAMCEF*

**Kilimo**: Milima ya Tao la Mashariki ni maarufu kwa kilimo kikubwa cha miti, mpunga, miwa na chai kutokana na kuwa na ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha na hivyo kusaidia kwa kiasi kikubwa katika kufikiwa kwa malengo ya Mikakati ya Serikali ya Kilimo Kwanza, Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (ASDP)

**Utalii:** Milima hii pia ni kivutio kikubwa cha utalii kutokana na kuwa na viumbe ndwele wengi na mandhari ya kuvutia. Misitu ya Mazingira Asilia ya Chome, Nilo, Magamba, Mkingu, Uluguru, Kilombero, Uzungwa Scarp pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa ni maeneo yenye vivutio vingi vya utalii yaliyomo katika Milima ya Tao la Mashariki.

**Mazao ya mbao na yasiyo timbao:** Misitu inayopatikana katika Milima ya Tao la Mashariki inazalisha mazao ya mbao na yasiyo timbao kama vile kuni, magogo yanayofaa kupasua mbao, madawa asili na matunda pori.

EAMCEF inafadhili miradi inayojihusisha na shughuli za maendeleo ya jamii, utafiti na uhifadhi na usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Shughuli hizo lazima ziwe zinalenga kuboresha uhifadhi wa bioanuwai na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo lengwa ya Milima ya Tao la Mashariki.

Mfuko huu umewezesha mafanikio makubwa katika utunzaji wa misitu iliyopo katika Milima ya Tao la Mashariki pamoja na ustawi na maendeleo ya jamii zinazoishi kandokando ya misitu hiyo. Kupitia ufadhili wa kifedha unaotolewa na EAMCEF miradi mingi imeanzishwa kupitia mbinu shirikishi ambazo zilitoa fursa mbalimbali kwa wanajamii kama vile wanawake, wanaume, wazee, watoto, vijana na watu wenye ulemavu kunufaika.

Mafanikio mengine ni: uanzishwaji wa miradi ya ujenzi wa majiko banifu, mipango ya matumizi bora ya ardhi, makinga maji, ufugaji (nyuki, ng'ombe na mbuzi wa maziwa, kuku, nguruwe, vipepeo na samaki); Kilimo (miti ya matunda, miti ya mbao, uyoga, alizeti, mahindi na maharage ya soya) na umewawezesha wanajamii kujiajiri na kujipatia kipato. Aidha, shughuli za ufadhili wa EAMCEF kwenye misitu ya hifadhi zimetoa fursa kwa wanajamii kupata ajira ambapo hujitengenezea mitaji ya biashara ndogondogo na kuinua hali ya maisha yao. Ufadhili wa miundombinu ya utalii kupitia EAMCEF huongeza idadi ya watalii na hivyo kuwanufaisha vijana kupitia shughuli za kuwahudumia na kuwaongoza watalii.



# SERIKALI YARASIMISHA MISITU 18 YA VIJIJI

*Na: Rahima Njaidi, MJUMITA*

Wizara ya Maliasili na Utalii imerasimisha misitu mipya 18 kuwa hifadhi za vijiji yenye ukubwa wa hekta 106,171.77 kupitia Tangazo la Serikali (GN) namba 540 la Septemba 02, 2022. Misitu hiyo inamilikiwa na Serikali za vijiji 17 katika Halmashauri za Wilaya za Tunduru, Kilwa, Liwale, Handeni na Kilindi. Urasimishaji wa misitu hii ni nyongeza kwenye Tangazo la Serikali la ***Misitu ya hifadhi katika ardhi ya vijiji namba 487 la mwaka 2020,*** ambalo ndiyo Kanuni Kuu ya kuanzishwa kwa misitu ya hifadhi ya vijiji. Kutokana na jitihada za Serikali za kuhakikisha kunakuwa na uendelezaji wa misitu katika ardhi za vijiji, kufikia mwezi Septemba, 2022, jumla ya misitu 97 ilikuwa imerasimishwa kupitia kanuni hii.

Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za Serikali kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Serikali ikiwemo Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na mashirika mengine kama Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Mendeleo (MCDI), Mfuko wa Uhifadhi Duniani (WWF) na Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC). Hatua hii ni sehemu ya jitihada za Serikali kufikia malengo ya kupunguza ufyekaji wa misitu ya asili nchini kwa asilimia 70 kutoka hekta 462,000 kwa mwaka kwa kuongeza misitu ya hifadhi ya vijiji kutoka hekta milioni 2.7 (mwaka 2021) hadi hekta milioni 16 ifikapo mwaka 2031 kama ambavyo Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu wa mwaka 2021 - 2031 unavyochanganua.

**Orodha ya misitu iliyotangazwa kwenye Tangazo la Serikali namba 540 la Septemba 02, 2022**

| Mkoa | Wilaya | Kijiji | Jina la Msitu | Ukubwa wa Msitu (ha) |
|---|---|---|---|---|
| Ruvuma | Tunduru | Ngapa | Mugalugalu | 16,855.20 |
| | | Sautimoja | Chihuruka | 21,966 |
| | | Machemba | Chiumbe | 4,612 |
| | | Namakambale | Ipapa | 4,491 |
| | | Songambele | Songolewa | 10,217.10 |
| | | Msinji | Malilima | 6,431 |
| | | Mindu | Liwina | 3,713 |
| Lindi | Kilwa | Nanjirinji B | Nanjirinji B | 5,971 |
| | Liwale | Kibutuka | Kinyororo | 5,654 |
| | | Ngongowele | Kiwiga | 6,475 |
| | | Ngongowele | Ndungutu | 5,474 |
| | | Litou | Mtamba | 1,805 |
| | | Mihumo | Machemekele | 1,805 |
| | | Mikuyu | Miwagilo | 1,373 |
| | | Ngunja | Nakawale | 6,557 |
| Tanga | Kilindi | Kwamwande | Matugusa | 920.23 |
| | | Kimbe | Kagali | 772.24 |
| | Handeni | Kwamsisi | Miwili | 1,080 |
| **Jumla** | | | **18** | **106,171.77** |




*Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mihima Mkoani Lindi akionesha ramani rasmi ya msitu wa hifadhi wa Kijiji*



*Wanawarsha wakimsikiliza Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii Mhe. CPA Mary Masanja (Mb)*

Wakati huo huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imehimiza ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Haya yalibainishwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii Mhe. CPA Mary Masanja (Mb), wakati akizindua warsha ya 22 ya MJUMITA iliyofanyika katika ukumbi wa Edema mjini Morogoro Novemba 15 na 16, 2022. Naibu Waziri alibainisha kuwa, Serikali imeweka sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali ambayo inatoa fursa kwa makundi yote ya kijamii kushiriki na kunufaika na usimamizi wa rasilimali za misitu. Alibainisha kuwa, Aprili, 2022 Serikali ilizindua rasmi Mpangokazi wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ambao unahamasisha ushiriki wa wanawake na vijana katika usimamizi wa misitu na kufanya maamuzi yanayohusu usimamizi wa misitu. Alisisitiza kuwa Mpango kazi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu wa mwaka 2021 - 2031, ambao uliandaliwa na kuidhinishwa na Serikali mwaka 2021.

“Lengo mojawapo la Serikali ni kuhamasisha na kuimarisha ushiriki wa wanawake na vijana kwenye shughuli za usimamizi wa misitu nchini, hivyo niwapongeze sana MJUMITA kwa kuleta dhima hii ambayo kwa kiasi kikubwa inahamasisha utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na miongozo ya kitaifa inayosimamia misitu nchini” alihitimisha Mhe. Masanja.



*Mtendaji Mkuu wa MJUMITA Rahima Njaidi akiongea na Wanawarsha*

# PFP2 YAONGEZA KASI YA UPANDAJI MITI KIBIASHARA

Na: Timu ya Waandishi, PFP2



Awamu ya pili ya Mradi wa *Panda Miti Kibiashara* ulioanza kutekelezwa Novemba, 2019 umebadilisha kwa kiasi kikubwa uwekezaji wa wadau wa upandaji miti katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikilinganishwa na kabla ya mradi kuanza. Awamu ya pili ya mradi huu itaisha Oktoba, 2023. Moja ya mafanikio ya awamu hii ya pili ni kuandaa mipango shirikishi ya utekelezaji wa mradi ambapo mradi kwa kushirikiana na Halmashauri 10 walichagua vijiji 80 kuwa eneo la utekelezaji. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Iringa ambapo vijiji 23 vimechaguliwa katika Halmashauri za Mufindi (15), Mfindi mji (3) na Kilolo (5); Mkoa wa Njombe ambapo jumla ya vijiji 53 vilichaguliwa katika Halmashauri za Njombe mji (7), Njombe (7), Ludewa (6), Makete 23 na Wanging'ombe 10; Mkoa wa Ruvuma vijiji vinne vilichaguliwa katika Halmashauri ya Madaba.

Mradi uliwezesha utayarishaji wa mwongozo wa uundaji na uendeshaji wa vikundi vya wakulima wadogo wa miti. Kazi hii ilifanywa kwa ushirikiano baina ya Mradi na Serikali za Mitaa katika kongani za Makete, Njombe na Mafinga. Mwongozo huu umesaidia wakulima kuwa na vikundi na umoja wao katika eneo la utekelezaji wa mradi.

Hadi Disemba 2022 vijiji vyote vinavyotekeleza mradi vimeunda vikundi. Vikundi vyote vimesajiliwa na mamlaka husika za serikali. Vikundi vyote 80, vina wanachama 3,846 (wanawake 1,365, wanaume 2,469 na asasi 12). Vikundi hivi vimeanza kutoa huduma ya jinsi ya kutunza mashamba ya miti, kwa wanachama wake na wasiokuwa wanachama.

Mradi pia kwa kushirikiana na wakulima wadogo na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umeendelea kuyasimamia mashamba 15 ya mbegu bora za miti. Kilo 35 za miti ya mipaina zimevunwa kutoka katika mashamba hayo.

Aidha, zaidi ya wakulima wadogo 30,000 wa miti wameshiriki katika mafunzo ya namna ya kuanzisha vitalu vya miti, kupanda miti, kupogolea na kupunguza miti, kufanya palizi na kuandaa njia za moto. Mradi umenunua na kugawa misumeno mchirizi (*pruning saw*) 400 na uliandaa mabango yaoneshayo namna ya kupunguzia na kupogolea miti kwa vikundi 80 katika vijiji vya mradi. Katika kuhamasisha upandaji miti wenye tija na wa kitalaam, mradi



*Magogo yaliyovunwa kutoka shamba la miti la mkulima mdogo wa miti*

umeanzisha mashamba darasa 115 katika vijiji 80 vya mradi.

Mradi pia umewezesha vijiji 19 kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Vilevile, jumla ya hati miliki za ardhi za kimila 869 zilitolewa kwa wakulima wa miti 277 na asasi 21 katika kijiji cha Ibaga Wilayani Makete.

Mbali na hayo mradi, umeiwezesha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kupitisha mitaala ya kufundishia wahudumu wa misitu na wachakataji wa mazao ya misitu. Mitaala hii imepitishwa na tayari mafunzo yameanza kutolewa kupitia vyuo vya ufundi stadi nchi nzima.

Mradi umesaidia wakulima wadogo 1,738 kuandaa mipango ya utunzaji wa mashamba ya miti. Zaidi ya Mashamba 1,782 yenye eneo la hekta 1,808.02 yamekamilisha mipango hiyo katika vijiji vyote 80 vya mradi.

Aidha, matanuru matano kutoka Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO) yamenunuliwa na kugawiwa kwa vikundi vitano vya wazalishaji wa mkaa Wilayani Makete. Tafiti zinaendelea kubaini changamoto na uwezo wa matanuru hayo katika kutengeneza mkaa. Mradi pia umeendelea kutoa elimu na teknolojia ya uzalishaji mkaa mbadala utokanao na mabaki ya mazao ya misitu.

Mradi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na wadau wengine umeandaa miongozo ya viwango vya ubora wa mbao na nguzo za miti. Viwango hivi vimetangazwa rasmi kupitia Tangazo la Serikali Namba 882 la Oktoba, 2020.


Mradi kwa kushirikiana na wadau umewezesha utekelezwaji wa Mwongozo Jumuishi wa Kusimamia Moto katika vijiji 80 vya mradi. Jumla ya maafisa ugani wa misitu na kilimo 206 wamepatiwa mafunzo maalum ya misitu hususan katika kuzuia na kupambana na moto.


Mradi pia umewezesha kuundwa kwa kamati 81 za moto na vikosi 81 vya kupambana na moto katika vijiji vya mradi. Vifaa vya kupambana na moto 800 na pampu 40 za kuzimia moto zimenunuliwa na kusambazwa katika vijiji vya mradi.

Mradi umewajengea uwezo wajasiriamali wadogo 4,750 kwa kuwapatia mafunzo ya namna ya kuchakata, kuzalisha mkaa, kunoa misumeno, kuendesha biashara na ufundi seremala.

Aidha, mradi umewezesha wakufunzi kutoka vyuo vya FITI, FTI na FWITC kuendelea kupata mafunzo ya taaluma ya ufundishaji hadi 2023. Mradi umenunua trekta na kontena maalumu lenye vifaa vya mafunzo ya misitu na viwanda vya misitu. Vifaa vimeanza kutumiwa katika kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wadau wanaofika katika Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu. Kituo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau na wafanyakazi wa viwanda vya misitu kulingana na mahitaji yao.

Haya ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha mwanzo cha utekelezaji wa mradi tangu kuanza kwake mwaka 2019. Aidha, yapo matarajio makubwa ya maboresho katika sekta ya misitu kupitia mradi huu ifikapo mwisho wa muda wa mradi Oktoba, 2023.



*Moja kati ya shamba la miti la mkulima mdogo wa miti*

# MAENDELEO YA PROGRAMU YA KUWEZESHA MNYORORO WA THAMANI WA UFUGAJI NYUKI NCHINI – BEVAC

*Na: Magdalena Muya, FBD*

Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Ufugaji Nyuki ilizinduliwa rasmi Februari 21, 2022 jijini Dodoma. Utekelezaji wa programu umejumuisha kipindi cha mpito cha miezi minne ambacho kiliisha Juni, 2022 ambapo tathmini za kuangalia mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki, mtazamo wa wateja wa ndani na nje ya nchi, mwenendo wa biashara ndogo na za kati za mazao ya nyuki na kipaumbele cha tafiti za ufugaji nyuki nchini Tanzania vimetekelezwa. Pamoja na tathmini hizo za kisayansi, programu pia iliangalia namna ya kufanya ukarabati wa maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori iliyopo Njiro jijini Arusha, kuimarisha miundombinu ya taasisi ikiwemo ujenzi wa bweni katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora.

Matokeo ya tathmini hizo yaliboresha shughuli zitakazotekelezwa katika kipindi chote cha mradi na kuainisha Wilaya ambazo shughuli hizo zitatekelezwa. Matokeo ya tathmini hizo yaliidhinishwa na kamati zote za mradi. Shughuli hizo ni kuwezesha: majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPD) ili kuainisha masuala na changamoto zinazohitaji maamuzi ya kisera; uandaaji mipango ya utekelezaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (2021 – 2031) na maandalizi ya Mikakati ya kukuza Sekta ya Ufugaji Nyuki Zanzibar.

Kazi nyingine ni; ujenzi wa bweni la wasichana na mapitio ya mitaala na mafunzo kwa wakufunzi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora; manunuzi ya vifaa vya maabara kwa ajili ya uchunguzi wa mazao ya nyuki katika Maabara ya Taifa ya Utafiti wa ufugaji nyuki iliyopo Njiro; uimarishaji wa uwezo wa vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki kwa kuvihamasisha kuungana ili kuwa na sauti moja yenye uwezo zaidi wa kukabiliana na changamoto zinazowakabili na urasimishaji wa maeneo ya masoko ya mazao ya nyuki jirani na maeneo yaliyohifadhiwa katika vijiji na kata.

Aidha, tafiti hizo zimebainisha kazi za: wachakataji wa mazao ya nyuki na upatikanaji wa vitendea kazi; utoaji wa elimu ya fedha na upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya mitaji; matumizi ya mitandao kwa ajili ya kupata taarifa muhimu za masoko kwa wafugaji nyuki na vikundi vya wazalishaji wa mazao ya nyuki; upatikanaji wa vifaa na teknolojia kwa ajili ya ufugaji nyuki kwa kuwaunganisha na masoko hayo; uanzishaji wa hifadhi za nyuki pamoja na uandaaji wa mipango ya usimamizi wa hifadhi hizo; utengenezaji wa chapa ya kitaifa ya mazao ya nyuki; utoaji wa elimu ya kuboresha biashara ya mazao nyuki na jinsi ya kuyafikia masoko ya nje ya nchi; na utoaji elimu na mafunzo kwenye uendelezaji, uboreshaji na uongezaji thamani ya mazao ya nyuki.

Wilaya 19 zimepitishwa kutekeleza shughuli za programu. Utekelezaji wa BEVAC utafanyika kwa kushirikiana na wataalamu wa Wilaya, Mikoa na Wizara zilizochaguliwa. Kati ya Wilaya zilichochaguliwa 15 ni za Tanzania Bara zilizopo mikoa ya Tabora (4); Singida (3); Shinyanga (1); Katavi (3) na Kigoma (4). Kwa upande wa Zanzibar Wilaya zote zilizochaguliwa zipo kisiwani Pemba katika mikoa ya Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Tangu shughuli zilipoanza kutekelezwa Julai Mosi, 2022 mikutano mbambali ilifanyika ambayo ililenga kuwajengea uwezo wadau wa sekta ya ufugaji nyuki. Mikutano hiyo ilikuwa juu ya mafunzo ya utetezi wa kibiashara, usimamizi wa ubora wa mazao ya nyuki kwa ajili ya kuuza nje na mafunzo ya kimkakati kwa vyama vya ushirika.

Aidha, programu imeanza kukusanya orodha ya maeneo yanayopendekezwa kuwa hifadhi na kanda za ufugaji nyuki. Kazi hii inalenga kuhakikisha maeneo ya ufugaji nyuki yanatambulika kisheria.

Lengo la programu ni kuhakikisha kuwa wadau wa sekta ya ufugaji nyuki watazitumia fursa zilizopo kwenye mradi ili kuongeza uzalishaji, ubora na masoko ya mazao ya nyuki kwa maendeleo yao binafsi na nchi kwa ujumla.

Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Ufugaji Nyuki ni mradi wa makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - (JMT) na Umoja wa Ulaya - (EU). Mradi huu ulisainiwa Septemba 17, 2020. Kipindi cha utekelezaji wa mradi cha miezi 72 kimegawanywa katika vipindi vidogo viwili ya miezi 48 na 24.

Shirika la Maendeleo la Ubelgiji - (Enabel) ndilo lililochaguliwa na EU kusimamia utekelezaji wa mradi kwa niaba ya umoja huo, wakati Wizara ya Maliasili na Utalii itatekeleza na kusimamia mradi kwa niaba ya Serikali ya Tanzania.



*Kiwanda kidogo cha uchakataji asali*

# SERIKALI KUIFANYA FTI KUJITEGEMEA KIUENDESHAJI

*Na: Christognus Haule, FTI*

Chuo cha Misitu Olmotonyi - (FTI) Disemba 03, 2022 kilifanya sherehe za mahafali ya 82 tangu kianzishwe. Hii inaonesha ukongwe na ubobezi wa chuo hicho katika kutoa mafunzo ya misitu na mazingira. Chuo kimekuwa kikipokea wanafunzi watanzania na wa nje ya Tanzania. Baadhi ya nchi zilizonufaika na mafunzo ya Chuo cha Misitu Olmotonyi ni Gambia, Comoro, Uswatini (Swaziland), Malawi, Zambia, Botswana na Siera Leon.



Katika mahafali ya mwaka huu, Mgeni Rasmi alikuwa ni Profesa Eliamani Sedoyeka, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye pamoja na mambo mengine aliwatunuku wahitimu 778 vyeti vya kumaliza mafunzo yanayotolewa na chuo.

Katibu Mkuu aliueleza uongozi wa chuo kuwa, lengo la Wizara ni kuendelea kukipanua chuo kwa kukiboresha kwa kukiwekea miundombinu ya kisasa ili hapo baadae chuo kiweze kujitegemea kiuendeshaji. Aidha, Profesa Sedoyeka alibainisha kuwa Moja ya mikakati ambayo chuo kinatakiwa kuwa nayo ni kuwa na programu mahususi ya kuwajengea uwezo wahitimu ili kujiajiri (*incubation programme).*" Alikipa chuo changamoto ya kuanzisha kiwanda cha mafunzo na ongezeko la idadi ya kozi kwa lengo la kuongeza wigo wa udahili wa wanafunzi."

"Mtazamo wa Serikali ni kukifanya chuo hiki kuwa kituo mahiri cha kutoa mafunzo ya misitu na mazingira katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika." Alisema Profesa Sedoyeka na kuongeza kuwa "Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, inayo matumaini makubwa kufikia ndoto hiyo."

Aidha, Profesa Sedoyeka aliwashukuru wadau mbalimbali wakiwemo Mfuko wa Misitu Tanzania - (TaFF) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - (TFS) kwa kufadhili ujenzi wa jengo la utawala ambalo limeboresha ufanisi na utendaji kazi wa watumishi na wanafunzi, pamoja na mandhari ya chuo.

Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI) ni moja ya vyuo vikongwe vilivyoanzishwa kabla ya uhuru wa Tanganyika. FTI ilianzishwa mwaka 1937 kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwa walinzi wa misitu (*Forest Guards*) kwa ajili ya uhifadhi wa misitu. Chuo cha Misitu Olmotonyi ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Chuo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi - (NACTVET) kwa namba REG/ANE/007. Chuo kina ithibati ya kutoa mafunzo ya kozi za Astashahada ya Awali ya Misitu (NTA 4-Basic Technician Certificate in Forestry), Astashahada ya Misitu (NTA 5-Technician Certificate in Forestry), Stashahada ya Misitu (NTA 6-Ordinary Diploma in Forestry), Stashahada ya Jioinfomatiki kwa Usimamizi wa Maliasili (NTA 6-Ordinary Diploma in Geoinformatics for Natural Resources Management) na Stashahada ya Misitu ya Mijini na Ustawishaji wa Mandhari (NTA 6-Ordinary Diploma in Urban Forestry and Landscaping).

# PLACES FOR ECOTOURISM IN TANZANIA – PART II

By: Staff Writer

Tanzania is among the best tourist destinations in the World. The country is endowed with a vast of natural biotic and abiotic tourism products ranging from plants, animals and physical features. Some of the tourism attracting features include the highest and lowest points of the African Continent, that is, the top of Mt. Kilimanjaro and the base of Lake Tanganyika respectively. The Government owns and manages most of these attractions while communities, individuals and villages manage a small part of the attractions. In recognition of the importance of these attractions; Tanzania has reserved one third of its land for conservation of forest, bees and wildlife. The Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT) manages these reserved lands through its government institutions namely: Tanzania Forest Services Agency (TFS), Tanzania Wildlife Management Authority (TAWA), Tanzania National Parks (TANAPA) and Ngorongoro Conservation Area Authority (NCAA). However, some are under the Local Government Authorities.

*Misitu ni Mali* welcomes you to some of the reserves endowed with eco-tourism attractions under the management of Tanzania Forest Services Agency. *Enjoy:*

## Amani Nature Reserve:



Amani Nature Reserve (ANR) is located in the Northeast corner of Tanzania within Muheza and Korogwe Districts in Tanga Region. The reserve covers 8,380 ha. Amani Nature Reserve is endowed with endangered species of both flora and fauna. The reserve is the home of Gentle and Colobus monkeys, Yellow baboons Chameleon and Butterfly, and Saint Paulia (African violets).

Amani Nature Reserve is suitable for camping, nature viewing, bird watching, walking safari and mountain hiking and biking.

The reserve is accessible by road via Muheza Township along Dar es Salaam - Tanga road. ANR is about 213 km from Tanga Municipal and 35 km from Muheza Township. The reserve provides limited accommodation, meals and drinks.

## Nilo Nature Forest Reserve:

Nilo Nature Forest Reserve (NNFR) is also located in Tanga Region in Korogwe, Muheza and Mkinga Districts. The Reserve is in Northwest of the famous East Usambara Mountains.

The unique natural features a tourist will enjoy while visiting the reserve include, the Holy water point, Tuvui waterfalls and Saint Paulia sites. Other attracting features are the Nilo and Lutindi peaks, which offer a best view of the East Usambara Mountains panorama. The nature reserve is suitable for trekking, bird watching, cultural tourism, biking, camping and research.



The area can be accessed by road either through Amani Forest Nature Reserve (35.1 km) or, via Korogwe Township (78.5 km) or via Maramba village (98 km). Accommodation and other social services are available in Tanga Municipality, and Korogwe and Muheza Townships

## Chome Nature Forest Reserve:

Chome Nature Forest Reserve (CNFR) is one of the most bio-diversified nature forest reserves in Tanzania. It is located in the South Pare Mountains in Northeast of Tanzania. It is the largest forest block in the South Pare Mountains covering an area of 14,283 ha.

The most prominent and unique feature in the reserve is the highest ridge of Mt. Shengena, which is 2463 a.m.s.l. The Nature Reserve is the best place for bird watching where a visitor can hear and watch the endemic forest birds like South Pare White- eye (*Zosterops winifridae*) and Hunter's cisticola (*Cisticola hunteri*). Other tourism attractions include small wild mammals like Yongoma and Thomson gazelle, waterfalls, closed montane forest, big tree of *Ocotea usambarensis,* Bat cave, sacred area, and historical and cultural value sites.



The reserve is suitable for hiking, bird watching, landscape viewing and research. CFNR is accessible via Same Township along the Dar es Salaam – Arusha road. The distance from Same – Mwembe - Vudee to Chome is 32 km. The road is passable throughout the year but require 4 Wheel Drive car. The reserve offers limited accommodation facilities, meals and drinks; therefore such services are available in Same Township.

## Magamba Nature Forest Reserve:

Magamba Nature Forest Reserve (MNFR) has an area of 9,283 ha and is located at Mlalo Division, Lushoto District in Tanga Region. The forest is beautified by undulating topography with a wide range of mountains coupled by a cool weather all the year around. During cold seasons, temperatures can go down to as 7°C.




Some of the tourism attractions in MNFR are the wide range of flora and fauna (plants, birds, butterflies and animals like and black and white collobus monkeys), historical and cultural features (old footprint and old German's cave), Sungi and Mkuzi waterfalls, skyline and Kiguluhakwea and Kwehondo viewpoints at which one can see Lushoto Township.

Visitors can camp for picnic, photographing and filming.

MFNR can be accessed through Dar es Salaam – Arusha road via Mombo and Lushoto Townships. Accommodation, meals and drinks are available at Lushoto Township.

### Uzungwa Scarps Nature Forest Reserve:



Uzungwa Scarps are in the Southern highlands of Tanzania in Iringa and Morogoro Regions, Kilolo and Mufindi Districts, and Kilombero District respectively. It is the largest mountain block of the Eastern Arc Mountains chain: rich in fauna species of high degree of endemism. The reserve is the home of 28 animal species.

One can reach the reserve through the Ipogoro route via Kilolo District (80 to 100 km from Iringa Municipality) or through Mufindi District route (130 km from Mafinga Town in Iringa Region. There is also the Mikumi route via Ifakara and Itongoa (80 km from Ifakara Township). There are campsites that can offer accommodation to few visitors.

### Kilombero Nature Reserve:



Kilombero Nature Reserve (KNR) is located in the Southwest highlands of Tanzania in the regions of Iringa and Morogoro in Kilolo and Kilombero Districts respectively. KNR is the largest mountain block of the Udzungwa Mountains with an area of 134,511 ha and International Union for Conservation of Nature (IUCN) categorised Kilombero Nature Reserve as a protected area managed for wildness protection.

The reserve is close to Mikumi, Udzungwa Mountain, Ruaha and Mwalimu Nyerere National Parks. Some of the tourism attractions in the nature reserve include the Kipunji monkey an endemic primate, Magombelema cave, Nyumbanitu peak and cultural activities of the Wahehe tribe.

One can reach the reserve from Dar es Salaam by road, air and train. Accommodation and other social services are available at the nearest villages and townships.

### Uluguru Nature Forest Reserve:



The Uluguru Nature Forest Reserve (UNFR) is very close to Morogoro Municipality. The reserve has an area of 24,115.09 ha. It is 180 km from Dar es Salaam, the biggest commercial city in Tanzania. One of the top priorities for biodiversity conservation in Africa; endowed with unique biodiversity richness and endemism for both flora and fauna.

Offers variety of attractions like; bird watching (Uluguru bushrike), waterfalls (Hululu), historical sites (German building), game view (White and Black collobus monkeys, Velvet monkeys) and traditional activities. Researches show that the reserve is a heaven for atleast 135 endemic plant species including rare African violets and orchid's resource.

The reserve is easily accessed due to its proximate to Dar es Salaam. Accommodation and other social services are available in Morogoro Municipality.

# FORVAC YAKAMILISHA ASILIMIA 90 YA MALENGO YAKE

*Na: James Nshare, FBD*



Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC), imekamilisha zaidi ya asilimia 90 ya kazi zilizopangwa tangu ilipoanzishwa kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2022. Aidha, kazi zilizobaki zitakamilishwa kwenye kipindi cha nyongeza cha programu cha miaka miwili (Julai, 2022 mpaka Julai, 2024). Jumla ya Euro milioni 4.2 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo hasa katika mikoa ya Ruvuma na Lindi. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kupitia programu hii ni pamoja na; kuandaliwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 41 ambapo zaidi hekta 268,517 zimetengwa kwa ajili ya kuhifadhi misitu. Mikoa iliyonufaika na kiasi cha hekta zilizotengwa kwa ajili ya hifadhi za misitu zikioneshwa kwenye mabano ni: Ruvuma (55,400), Lindi (194,912) na Tanga (18,205.81).



*Wanafunzi wakishiriki katika zoezi la upandaji miti*

Mafanikio mengine ni kuundwa na kuhuishwa kwa kamati 94 za maliasili za vijiji (VNRCs) katika mikoa ya Ruvuma kamati 34 kati ya 41; Lindi kamati 34 kati ya 45 na Tanga kamati 26 kati ya 29. Mikoa hiyo pia imenunuliwa jozi 395 za sare kwa ajili ya kamati za mazingira za vijiji. Vijiji 11 vya Mkoa wa Lindi vilinunuliwa jozi 181, Tanga jozi 44 kwa ajili ya vijiji vinne na Ruvuma jozi 170 kwa ajili ya vijiji 10.

Programu pia imeinunulia mikoa hiyo jumla ya pikipiki 37 kwa ajili ya VNRC na ofisi za Halmashauri za Wilaya.

Pikipiki hizo zitasaidia usimamizi wa shughuli zote za misitu ya vijiji. Mkoa wa Ruvuma umenunuliwa pikipiki 14, nne zikiwa zimegawiwa vijijini kwa ajili ya doria na kumi kwa ajili ya maafisa ugani wa Halmashauri za Wilaya kama inavyoonekana kwenye jedwali namba moja.

**Mgawanyo wa Pikipiki Mkoani Ruvuma**

| Wilaya | Vijijini | Wilayani |
|---|---|---|
| Songea | 1 | 2 |
| Mbinga | 0 | 2 |
| Nyasa | 1 | 2 |
| Tunduru | 1 | 2 |
| Namtumbo | 1 | 2 |
| **Jumla** | **4** | **10** |

Mkoa wa Lindi umepata pikipiki 16; Pikipiki 12 kwa ajili ya Kamati za mazingira za vijiji na nne kwa ajili ya maafisa misitu na nyuki wa Halmashauri za Wilaya. Mgawanyo wa pikipiki hizo unaoneshwa kwenye jedwali namba 2.

**Mgawanyo wa Pikipiki Mkoani Lindi**

| Wilaya | Vijijini | Wilayani |
|---|---|---|
| Ruangwa | 3 | 2 |
| Liwale | 5 | 1 |
| Nachingwea | 4 | 1 |
| **Jumla** | **12** | **4** |

Pikipiki saba zilinunuliwa kwa ajili ya mkoa wa Tanga kati yake nne ziligawiwa vijijini kwa ajili ya VNRC na tatu zilipewa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya maafisa ugani wa misitu na nyuki. Mgawanyo wake unaoneshwa kwenye Jedwali namba 3.

**Mgawanyo wa Pikipiki Mkoani Ruvuma**

| Wilaya | Vijijini | Wilayani |
|---|---|---|
| Handeni | 3 | 1 |
| Kilindi | 1 | 1 |
| Mpwapwa | 0 | 1 |
| **Jumla** | **4** | **3** |

FORVAC pia imesaidia katika maandalizi ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu 46 na sheria ndogo za usimamizi misitu ya vijiji. Kwa ujumla mipango yote imehusisha hekta 316,390 za misitu ya vijiji (VLFRs).

Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya vijiji na sheria ndogo nane zimeandaliwa katika Mkoa wa Ruvuma. Wilaya ya Songea mipango minne na sheria ndogo nne, Wilaya ya Namtumbo Mpango mmoja na sheria ndogo moja na Wilaya ya Tunduru Mipango mitatu na sheria ndogo tatu. Mipango yote inajumuisha eneo la misitu ya vijiji la hekta 55,511. Aidha, mipango hiyo imejumuisha mita za ujazo ($m^3$) 11,711 ambazo ziko tayari kuuzwa kwa wadau. Vijiji vya Ndongosi na Litowa katika Wilaya ya Songea vimeshaanza kuvuna miti katika hifadhi za misitu za vijiji vyao.

Katika Mkoa wa Lindi Mipango ya usimamizi 34 na sheria ndogo za vijiji 31 zimeandaliwa. Wilaya ya Ruangwa imeandaliwa mipango mitano na sheria ndogo tano, Wilaya ya Liwale Mipango 19 na sheria 16 wakati Wilaya ya Nachingwea imeandaa mipango 10 na sheria ndogo 10. Mipango yote hiyo inajumuisha eneo la misitu ya vijiji (VLFRs) la hekta 249,608.70 na kiasi cha mita za ujazo ($m^3$) 66,904 zinaweza kuvunwa. Aidha, vijiji 15 vimeanza kuvuna miti katika misitu yao.

Mkoa wa Tanga ambao kongani yake hujumuisha na Wilaya ya Kiteto imeandaa Mipango ya Usimamizi wa Misitu mitano na sheria ndogo 17. Wilaya ya Handeni imeandaa Mipango mitatu na sheria ndogo tatu, Wilaya ya Kilindi Mpango mmoja na sheria ndogo moja wakati Wilaya ya Kiteto imeandaa Mpango mmoja na sheria ndogo 13. Mipango yote hiyo imehusisha hekta 11,270 za misitu ya vijiji na mita za ujazo 1,951 zinaweza kuvunwa. Aidha, vijiji vya Mkonde na Gole vya Wilaya za Kilindi na Handeni mtawalia vimeanza uvunaji.

Programu ya FORVAC ilianzishwa kwa malengo ya; kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo huo; kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira zinazotokana na misitu ya asili na kupunguza uharibifu wa misitu; kuimarisha uwezo wa wadau; kuendeleza elimu ya ugani, ufuatiliaji na tathmini na kuanzisha mifumo ya TEHAMA; na kuwezesha Wizara katika uandaaji wa sera, sheria na miongozo.

Kazi zilizofanyika ni: kuanzisha na kuhamasisha uanzishwaji wa Hifadhi za Misitu ya Vijiji (VLFRs), kuwezesha uongezaji thamani wa mazao ya misitu, kuimarisha usimamizi wa misitu ya jamii (CBFM) na kuboresha uwezo wa kitaasisi na usimamizi wa Halmashauri za Vijiji na Kamati za Maliasili za Vijiji (VNRC) ili ziweze kutekeleza dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika kutenga misitu yao na kuisimamia ipasavyo, pamoja na kuboresha uwezo wa kusaidia na kufuatilia shughuli za usimamizi wa misitu hiyo ya jamii.

Kazi nyingine ni kuboresha mitaala ya vyuo vinavyotoa taaluma ya misitu, kama vile Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI), Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora (BTI) na Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Mbao (FWTIC) kwa kujumuisha masuala ya mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu, mifumo ya masoko na ujuzi wa namna ya kukuza biashara.

Aidha, kuimarisha huduma za ugani na mawasiliano; kuanzisha Mfumo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Usimamizi (MIS); kuboresha sera na mifumo ya udhibiti wa maendeleo ya mnyororo wa thamani wa misitu; na kuwezesha kuimarisha mifumo ya kusimamia utekelezaji wa sheria ya misitu, utawala bora wa misitu na biashara ya mbao zinazopatikana kisheria.




*Makabidhiano ya pikipiki zilizonunuliwa na mradi*



*Mgeni rasmi Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Prof. Eliamani Sedoyeka akitoa hotuba ya mkutano kufuatia mapendekezo ya wadau wa sekta ya ufugaji nyuki*

# SERIKALI - WADAU KUIMARISHA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI NCHINI

*Na: Imelda Emmanuel, FBD*

Katika kutambua mchango wa wadau kwenye uendelezaji wa sekta ya ufugaji nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanya mkutano wa siku mbili na wadau wa sekta ya ufugaji nyuki kuanzia Novemba 29 hadi 30, 2022 jijini Dodoma. Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki takriban 75 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki, Bw. Deusdedit Bwoyo aliwaambia wadau hao kuwa lengo la mkutano huo ni kujadili maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki, kutoa mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta na kuiwezesha sekta kuongeza kiwango cha asali kinachozalishwa ili kukidhi soko la ndani na nje ya nchi.

Mkutano huo ulitoa fursa kwa serikali na wadau kujadili na kutoa maoni katika maeneo mbalimbali yakiwemo: hali ya sekta ya ufugaji nyuki nchini; changamoto za kufanya biashara ya mazao ya nyuki ndani na nje ya Tanzania; vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki; viwanda vya sekta ya ufugaji nyuki; tafiti, mafunzo na huduma ya ugani kuwa ufugaji nyuki; mifumo ya masoko na ufuatiliaji wa ubora wa mazao ya nyuki.

Akitoa wasilisho la hali ya sekta ya ufugaji nyuki nchini, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Uendelezaji Ufugaji Nyuki, Idara ya Misitu na Nyuki Bw. Daniel Pancras alieleza kuwa moja ya jitihada ambazo serikali inazifanya katika kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki nchini ni kuandaa na kusambaza miongozo mbalimbali inayowezesha usimamizi wa sekta. Miongoni mwa miongozo iliyotolewa na Wizara ni mwongozo wa kitaifa wa mafunzo na elimu ya ugani ya Ufugaji nyuki wa mwaka 2020 (*National Bekeeping Training and Extension Service Guideline 2020).* Mwongozo huo ni kama kitini cha namna ya kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu ufugaji nyuki. Mkurugenzi Daniel alitoa rai kwa wadau wote kutumia mwongozo huo ili kuhakikisha kuwa huduma ya ugani na mafunzo yanayotolewa kwa wafugaji nyuki na wadau wengine yanakidhi viwango vinavyohitajika. Pia, aliwakumbusha wadau wote wanaojihusisha na kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki kuwasilisha taarifa zao Wizarani kabla ya Disemba 30, 2022 kwa ajili ya utambuzi na ufuatiliaji.

Aidha, Mwenyekiti wa Taasisi ya API-SUPPORT Bw. Linus Gedi alitoa wasilisho kuhusu changamoto za kufanya biashara ya mazao ya nyuki ndani na nje ya Tanzania. Katika wasilisho lake Bw. Gedi aliiomba serikali kuangalia na kupitia upya wingi wa tozo wakati wa usajili wa biashara ya mazao ya nyuki na upatikanaji wa vibali vya kusafirisha mazao hayo.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa sekta ya ufugaji nyuki, Bw. Seif Salum, Afisa ufugaji nyuki kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya



*Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki Bw. Deusdedit Bwoyo akifungua Mkutano wa Wadau Sekta ya Ufugaji Nyuki 29 Novemba, 2022 jijini Dodoma.*

Tabora aliishukuru Wizara kwa kuona umuhimu wa kuwakutanisha wadau kujadili masuala muhimu yanayoihusu sekta. Pia aliwasilisha mapendekezo ya wadau ikiwa ni pamoja na kuiomba Serikali ifanye taratibu za kuwezesha asali kuwa mojawapo ya zao la kimkakati ili kuweza kutatua changamoto ya mifumo ya masoko, upatikanaji wa takwimu, ubora wa asali na



*Wadau wakiwa katika mkutano wakisikiliza hoja na mapendekezo kwa maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini*

masuala mengine yanayokwamisha maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini. Aidha, aliitaka serikali iangalie namna ya uendeshaji wa viwanda vilivyopo na vituo vya kukusanyia mazao ya nyuki viendeshwe kwa mfumo wa ubia baina ya serikali na sekta binafsi ili kupunguza mzigo kwa serikali na kuongeza ufanisi wa viwanda hivyo.

Bw. Seif Salum pia alieleza kuwa kilio cha wadau wengi wa ufugaji nyuki ni uvamizi wa maeneo wanayotumia katika ufugaji nyuki. Hivyo, wanaomba serikali kuanzisha kanda za ufugaji nyuki katika hifadhi za misitu ili waweze kupata maeneo ya kufanya shughuli zao bila kuingiliwa na shughuli nyingine. Sambamba na hilo aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha na kurasimisha vitalu vya ufugaji nyuki katika maeneo ya hifadhi za misitu na mapori ya akiba ambapo mfugaji nyuki, kampuni, vyama vya ushirika au vikundi vya ufugaji nyuki wanaweza kupatiwa kitalu husika kwa makubaliano maalum na uongozi wa hifadhi hizo kwa ajili ya kufanya shughuli za ufugaji nyuki.

Aidha, alieleza kuwa uoto wa asili wa Itigi *thickets* uliopo Wilaya ya Manyoni unaendelea kupotea kutokana na shughuli za kibinadamu hususani kilimo cha korosho, hivyo aliiomba serikali kutofumbia macho suala hilo kwani uoto huo una mimea muhimu katika ufugaji nyuki, hivyo ni muhimu serikali kuangalia namna ya kuuhifadhi kwa kutenga maeneo hayo ili yaweze kutumika kama hifadhi za nyuki.

Akihitimisha wasilisho lake Bw. Seif alisisitiza suala la utafiti wa nyuki, alisema kuwa wadau wanatambua juhudi za wizara katika suala zima la kufanya tafiti za ufugaji nyuki. Hivyo ni vyema matokeo ya tafiti zinazofanywa kusambazwa kwa wadau katika lugha rahisi ili waweze kunufaika na tafiti hizo. Na mwisho aliomba serikali kuanzisha utaratibu wa kutoa tuzo au zawadi kwa wadau wanaofanya vizuri katika sekta ya ufugaji nyuki ili kuwapa hamasa na kuvutia wadau wengi zaidi waweze kujihusisha na shughuli za ufugaji nyuki.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na utalii Prof. Eliamani Sedoyeka ambaye alikuwa mgeni rasmi wakati wa kufunga mkutano huo, alieleza kuwa, kwa kipindi kirefu ufugaji nyuki umekuwa ukifanyika kwa njia za asili ambapo takribani asilimia 90 ya mizinga ni ya magogo na magome ya miti na katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia taasisi zake zikiwemo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Mfuko wa Misitu Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na miradi mbalimbali ya wizara imekuwa ikiwapatia wafugaji nyuki vifaa kama vile mizinga, mavazi ya kujikinga na vifaa vya kuchakatia asali kwa lengo la kuhamasisha matumizi endelevu ya teknolojia bora katika mnyororo wa kuongeza thamani ya mazao ya nyuki.

Prof. Sedoyeka aliongelea pia suala la masoko ya mazao ya nyuki na kufafanua kuwa, katika soko la nje kuna uhitaji mkubwa wa mazao ya nyuki hasa mazao ambayo ni mahuluku (*organic)* hivyo, ni vyema kuzalisha mazao yenye ubora na kukidhi viwango vya kimataifa ili kunufaika na soko hilo. Aidha, aliongeza kuwa, serikali imefanya juhudi za kutafuta soko la asali nchini China, na ipo katika hatua za mwisho za kuweza kukubaliwa kupeleka asali katika nchi hiyo.

Pia, aliielekeza TAFORI kushirikiana na vyuo vinavyojihusisha na ufugaji nyuki kuweza kufanya tafiti zitakazoibua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya ufugaji nyuki.

Mwisho Prof. Sedoyeka aliwahakikishia wadau kuwa wizara itaendelea kushirikiana nao katika kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji na ukuaji wa sekta na kuchangia katika kukuza kipato cha wananchi na Taifa kwa ujumla na kuwa masuala yote waliyopendekeza katika mkutano huo yanawezekana na yatafanyiwa kazi ipasavyo.

# MOUNTAIN RUNGWE NATURE FOREST RESERVE (MRNFR) PROFILE

*By: Petro Mholage, FBD*

**Introduction**

Mountain Rungwe Nature Forest Reserve (MRNFR) is among of the Nature Forest Reserves found in Mbeya Region in the Southern highlands of Tanzania. Apart from MRNFR other nature forest reserves are Uzungwa, Kilombero and Kalambo. MRNFR is a famous world biodiversity hotspot, which is rich in flora and fauna, historical and cultural values, and beautiful landscapes. Mountain Rungwe nature forest reserve covers 24,680.5 ha. The forest reserve is a home of species of more than 460 plant, 85 mammals, 230 birds, 32 reptiles, 36 amphibians, 10 fish and 283 butterflies. At least 42 of these species are endemic. Mountain Rungwe is a dormant volcano that stands at the junction of the eastern and western arms of the great lift valley. The climb is beautiful rewarding and as on clear days Lake Nyasa and the Livingstone Mountains can be seen to the southeast. Mountain Rungwe joins Kitulo National Park to the east and the World Conservation Societies managed Nkuka Forest to the southwest, nearby are scattered forest areas known as *Masieto* that are traditionary respected and used by local Nyakusa, Safwa and Kinga communities for worshipping.

**The History of Mountain Rungwe Nature Forest Reserve**

Mount Rungwe Nature Forest Reserve has a long history that dates back to 1949 when it was first gazetted as a Catchment Forest with an area of 13,652.1 ha. It is a tropical montane forest with unique species composition, structure and biodiversity. The reserve is an important conservation area in Tanzania as well as having great values at regional and global levels. In 2009 the reserve was upgraded to a nature forest reserve so as to improve its conservation. The main vegetation types of the reserve are lower montane forest, upper montane forest, bushed grassland, bamboo belt (covers 866 ha of a total size at altitude 2600 a.m.s.l), and heath.

**Importance of MRNFR**

The reserve offers diverse choices of activities including recreational activities, adventures, scientific research and educational activities. The most special features of MRNFR are the opportunity to gain a wide range of recreation choices and experience mainly from natural features including flora and fauna, landscapes, rocks, mountain peak, streams, rivers, and cultural and historical features like Lusiba Lwamisi, Lusiba Lukafu, and Pavala lutali craters and Lake Ngosi Crater. Other recreation choices are local brew making, traditional dances, historical churches and Lakes. Most of these attractions are found inside the reserve and some outside.

Mount Rungwe offers a diverse of unique scenery featuring Rungwe Peak (2,981 a.m.s.l), Experienced hikers who start early can hike it in a day, a barren mountain top from which one can view Poroto Ridge, Mbeya Peak, Loleza (Kaluwe) Peak and areas stretching down into Malawi. These attract an array of mountain hikers and climbers. Another feature of interest is a Crater Lake Lusiba found below the bamboo belt at 2,400 m a.s.l.. Lusiba-lukafu is an evergreen seasonal stream.

Mount Rungwe Nature Forest Reserve is key in conservation of residual tropical montane forest as well as rare, endemic and endangered biodiversity. It is a reservoir of species heritage in Tanzania and the world at large. The Reserve hosts two of the world's twenty-five most rare primates, the Kipunji (*Rungwecebus kipunji*) and the *Colobus guereza*. The reserve also harbours one of the rare antelopes - *Abbott's duicker*. The Reserve is a key water tower in the region providing water to countless villages and towns for domestic, agriculture and industrial uses in Mbeya, Rungwe and Kyela Districts. The mountain is a key water source of rivers of Kiwira, Suma, Mbaka, Kilasi, Marogala, Mrombo, Mulagala, Sinini and Mwatisi, which flow into Lake Nyasa shared by Tanzania, Malawi and Mozambique.

In the nearby Kiwira valley you'll find a unique natural bridge, named the Daraja la Mungu literally the God's Bridge. Also not too far away is Lake Ngosi, nestled in a volcanic crater in the Poroto Ridge Forest Reserve.

**Plants in MRNFR**

More than 300 plant species are found within MRNFR. Dominant plant species include *Aphloia theiformis, Ficalhoa laurifolia, Maesa lanceolata, Trichocladus ellipticus, Albizia gummifera* and *Bersama abyssinica, Macaranga conglomerata, Vepris nobilis, Syzgium guineense, Dasylepis integra, Flacourtia indica* and *Psychotria goetzei, Ficus sur, Bridelia micrantha.*

**Trees with their benefits**

Communities close to the MRNFR benefit from various plants species located in the reserve including; Used as source of drinking water in the forest - wild banana *Ensete ventricosum*, many of plants are used in curing various diseases example *Maesa lanceolata* used as traditional medicine against bacterial infections in the small intestine and viral infections in the liver and throat, as well as treatment for rheumatic arthritis, *Macaranga conglomerate* used traditionally treating coughing, fungal infection, and wounds *Vepris nobilis* is used in treatment of pneumonia, rheumatism and itching *Syzygium guineense* used in treating coughs, asthma, throat problems and intercostal pain in Cameroon the bark is used for the treatment of snakebites, some of plants species used as repelants to snakes - *Polyscias fulva,* most of plant species yield fruits for wild animals including monkeys and human being (*Myrianthus holstii*, *Tabernaemontana stapfiana, Ensete ventricosum),* Create attractive environment with best breathing interested air, Create an ecosystem as habitat



*Rungwecebus kipunji*

where abundant Wild organism's dwells and also contributes to water conservation there is interested water falls inside Mountain Rungwe Nature Forest Reserve.

**Main Tourism Attractive Features of Mountain Rungwe Nature Reserves**

**Presence of Mountain Rungwe**
Mountain Rungwe is located in Mbeya region at Rungwe District. It has height of 2,981 metres from the sea level to its top. About 75% of Mountain Rungwe is covered with thick montane forest.

**Presence of Lake Ngosi** in Poroto Ridge Forest Reserve, Features of Lake ngosi include the following: its top view shows a map of Africa. It has 74 metres depth.

**Presence of *Rungwecebus kipunji*,** The Nature Reserve is a significant ecological area that protects the endangered *Rungwecebus kipunji*.

**Presence of Birds**
MRFNR has more than 230 bird species including; Blue swallow *Hirundu atrocaerulea*, Iringa akalat *Sheppardia lowei*, Kipengere seedeater *Serinus melanochrous*, Uhehe fiscal *Lanius marwitzi*, Mountain marsh widow bird *Euplectes psammocromius* to mention few.

**Presence of Water Falls**
While being at the mountain Rungwe one will be abe to see Water falls

**Presence of Chameleons**
Uporoto horned chameleon *Chameleo fuelleborni*, Ukinga hornless chameleon *Chameleo incornutus*, Tubercle-nosed chameleon *Chameleo tempeli*, Pitless pygmy chameleon *Rhampoeon nchisiensis*, Rosette-nosed Chameleon (*Rhampholeon spinosus)*, Matschie's two-horned Chamaeleon (*Kinyongia matschiei*), Vosseler's Blade-horned Chameleon (*Kinyongia vosseleri)*, Matschie's Dwarf Chameleon (*Kinyongia tenuis).*

The MRNFR is in Rungwe district, Mbeya region, Southwest Tanzania and located between 90 03' - 90 12'S and 330 35' - 330 45'E. Regionally Rungwe district borders Kyela district in the South, Ileje district in West, Makete district in East and Mbeya district in North.

**Access**
The reserve is 25 km southeast of the regional centre, Mbeya town, and 7 km north of Tukuyu. The reserve can be accessed in the north and east via the Isongole-Ndala road (Ngumbulu-road), which runs between the reserve boundary and Kitulo National Park. In the West, the area is serviced by the Rungwe Mission road, which runs along the reserve boundary in several places. In the South, access to the reserve is by the Katumba-Kandete road and 10 km to the northwest is the Poroto Ridge Forest Reserve with impressive Crater of Lake Ngosi.

**When to visit mount Rungwe nature forest reserve**
The reserve is accessible throughout the year because infrastructures are well maintained. The best time to visit Mount Rungwe Nature Forest Reserve is around 07.00a.m in the morning to 06.30p.m in the evening during dry season June to October. The time is good for bird watchers, nature lovers and adventurers. At that time visitors can enjoy beautiful scenery of the reserve including varieties of plants, Crater Lakes including Lake Ngosi, chameleons, black and white colubus monkeys, Vervet monkeys, ants, spiders, and snakes, birds, streams scenery, mountain peaks, villages, historical sites, ritual sites and cultural activities. Moreover, night walk is also allowed inside the reserve. During long rain season from February-May and short rain season from October-December visitors are advised to carry special hiking gears including raincoats, rain boot and umbrellas.

**Areas of Interest to visit when visiting Mountain Rungwe Nature Forest Reserve**
Visiting mount Rungwe you will also be able to see Lake Ngosi, Rift Valley Meeting point, God's Bridge, Matema Beach, Kitulo National Park, Hot springs, Kapologwe water falls, Mt Livingstones Forest Reserve, Lake Masoko and Meteorite in Mbozi.

**Lake Ngosi**
Lake Ngosi is the second largest Crater Lake in Africa, which is found near Tukuyu, a small town in the highland Rungwe District, Mbeya Region, of southern Tanzania in East Africa. It is only 10.7 Kilometers to Lake Ngosi via Kyela road. It happened as result of volcanic eruption happened millions of years back. Lake Ngosi is part of the Poroto Mountains within the Mountain Rungwe Nature Forest Reserve. Areas on the Poroto Mountain have Forest known as Poroto Forest the forest together with lake Ngosi are part of Mountain Rungwe Nature Forest Reserve. Its water appearance changes from blue, green and deep blue colour. It has a unique appearance which shows the map of Africa. It has 74 meters depth, there is no river that takes water in or out of Lake Ngosi. It have 2.5 km longest length and 1.6 km shortest width making an area of 3.1 $Km^2$. Poroto forest which is surrounding the Lake Ngosi consist of abundant Plant species including Wild banana (*Ensete ventricosum*), *Ilex mitis,* and *Bamboo spp.*

**Communities' economic activities**
People of Rungwe District benefit from the Mountain Rungwe Nature Forest Reserve by various ways including practicing agriculture cultivating various crops Tea, Banana and Avocado. Others engage in Tour guiding activities and Forest plantation business.




# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII YABORESHA MIUNDOMBINU YA CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU

*Na: Dkt. Joseph Makero, FITI*

Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania imeendelea kuboresha miundombinu ya Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI). Chuo cha Viwanda vya Misitu ni chuo pekee nchini kinachotoa mafunzo ya viwanda vya misitu. Katika kupunguza changamoto za uchakavu wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ya chuo, Wizara imewezesha miradi mikubwa minne ambayo imesaidia kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo na kuwajengea wakufunzi uwezo na tija katika kutoa mafunzo.

Katika kipindi cha miaka mitano (2017 - 2022) Wizara imewezesha miradi ya;

**Ujenzi wa jengo la maktaba na maabara:** Mradi huu ulianza mwaka 2017 na kukamilika mwaka 2019. Lengo la mradi ni kupunguza changamoto ya ofisi kwa wakufunzi, vyumba vya mikutano, ukosefu wa maabara ya kompyuta na mbao, na maktaba kwa ajili ya watumishi na wanafunzi. Wizara kupitia taasisi zake imetoa ruzuku iliyotumika kujenga jengo hilo. Jengo limeanza kutumika kwa ajili ya mafunzo, utawala, mikutano na huduma za ugani. Jumla ya wakufunzi nane wamepata ofisi katika jengo hilo. Aidha, wanafunzi 100 wanaweza kukaa katika chumba cha maktaba kwa wakati mmoja. Pia, wanafunzi 30 wanaweza kutumia vifaa vilivyopo maabara ya kompyuta na mbao kwa wakati mmoja.

**Mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani wa mabaki yatokanayo na mazao ya mbao na utafutaji wa masoko ya mazao ya misitu:** Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2019. Lengo la mradi ni kuongeza wigo wa bidhaa zitokanazo na mbao na kutafuta masoko ya bidhaa hizo. Wizara imetoa ruzuku kwa ajili ya kununua mtambo wa kuunganisha vipande vya mbao na kutengenezea bidhaa mbalimbali za mbao. Kupitia mradi huu, chuo kimewajengea uwezo baadhi ya wakufunzi na mafundi sanifu katika kuongeza mnyororo wa thamani wa mabaki ya mbao kutokana na kazi za useremala. Takribani miradi minne ya utengenezaji wa samani imetekelezwa na chuo kati ya Julai na Disemba, 2022 na ilitumia teknolojia hii na hivyo, kuongeza mnyororo wa thamani wa mabaki ya mbao ambayo yangechomwa au kutupwa.

**Mradi wa ununuzi wa vifaa vya maktaba na maabara:** Mradi huu ulitekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Lengo la mradi ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Takribani aina nne za samani, vifaa saba vya maabara na vifaa vitatu vya ofisi vilinunuliwa. Kupitia mradi huu chuo kimeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kimewajengea uwezo baadhi ya wakufunzi kutoa mafunzo ya upimaji wa uimara na ubora wa mbao kwa tija.



**Mradi wa ununuzi wa usafiri kwa ajili ya jumuiya ya chuo:** Mradi huu umetekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Mradi ulifanikisha kununuliwa kwa basi kwa ajili ya safari za mafunzo za wanafunzi na watumishi wa chuo. Chuo kimepata basi hilo ambalo linauwezo wa kuchukua abiria 30 kwa wakati mmoja. Upatikanaji wa basi hilo umepunguza changamoto ya usafiri kwa wanafunzi na wakufunzi hasa wakati wa mafunzo nje ya kampasi.

Faida ya jumla ya maboresho ya miundombinu ya chuo ni kuongezeka kwa tija katika utoaji wa mafunzo, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi na wahitimu wa fani ya viwanda vya misitu. Katika mwaka wa masomo 2022/2023, wanafunzi 309 wamedahiliwa, hili ni ongezeko la wanafunzi 251 ukilinganisha na wanafunzi 58 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2014/2015. Aidha, idadi ya wahitimu imeongezeka kutoka wahitimu 28 mwaka 2015 hadi kufikia wahitimu 135 mwaka 2022.

Katika mahafali ya 25 mgeni rasmi Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya



*Baadhi ya wahitimu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu katika mahafali ya 25*

Maliasili na Utalii, Bw. Juma Mkomi, aliwataka wahitimu kuwa mabalozi wazuri wa chuo ili kuvutia waombaji wengi kuja kupata maarifa na ujuzi wa matumizi endelevu ya mazao ya misitu. Katika kuunga mkono juhudi za Wizara kuboresha mazingira ya chuo, chuo kina mpango wa kuanza programu ya kuatamia wanafunzi (*Incubation program*) ili kuwajengea uwezo wahitimu waweze kujiajiri na kuajirika. Pia chuo kitaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya misitu ili kuboresha miundombinu ya chuo kwa ajili ya kuongeza tija katika utoaji wa mafunzo ya viwanda vya misitu na matumizi endelevu ya mazao ya misitu nchini.

Kwa mawasiliano zaidi kuhusu mafunzo na huduma nyingine zinazotolewa na Chuo wasiliana na;

Ofisi ya Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Viwanda vya Misitu,
S.L.P 1925, MOSHI.
Simu: +255 (0) 787 676984 au
+255 (0) 787676981
Barua pepe: fiti@maliasili.go.tz




# WEKEZENI KWENYE VIWANDA VYA KUCHAKATA MAZAO YA NYUKI – PROFESA SEDOYEKA

*Na: Daud Semu, BTI*

Wadau wa sekta ya ufugaji nyuki wamehimizwa kuwekeza kwenye viwanda vya kuongeza thamani mazao ya nyuki. Akiwahutubia wahitimu wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora (BTI), Mgeni rasmi katika mahafali ya mwaka 2022 Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Profesa Eliamani Sedoyeka alisema, “Kwa kuanzisha viwanda vya uchakataji wa mazao ya nyuki kutasaidia katika kuzalisha asali bora na inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa na hivyo kuongeza ajira kwa vijana.” Aidha, Katibu Mkuu aliwataka wadau wa sekta ya ufugaji nyuki kutumia fursa zilizopo kwenye mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Ufugaji Nyuki nchini *(*BEVAC*)* ili kujijengea uwezo na kujitangaza.

Chuo hufanya mahafali kila mwisho wa mwaka wa masomo. Novemba 11, 2022 chuo kimefanya mahafali ya 11 yenye kauli mbiu “**Nyuki ni Uchumi, Tuwatunze watutunze – Kazi iendelee.”** Katika mahafali hayo, mgeni rasmi aliwatunuku vyeti na zawadi wahitimu 270. Wahitimu 170 walitunukiwa Astashahda ya Ufugaji Nyuki (*Technician Certificate in Beekeeping*) na 100 walitunukiwa stashahada ya Ufugaji nyuki (*Ordinary Diploma in Beekeeping*).

BTI ni chuo pekee cha kiserekali nchini Tanzania kinachotoa mafunzo kwa fani ya ufugaji nyuki kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada pamoja na kozi za muda mfupi. Chuo kipo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kinapatikana mkoani Tabora takribani kilometa nne kutoka Tabora Mjini. Uwepo wa chuo katika ukanda wa Miombo unafanya shughuli za mafunzo kuwa fanisi na hivyo kujihakikishia ubora wa mafunzo yanayotolewa. Kwa kutambua umuhimu wa ufugaji nyuki katika kupunguza umaskini na kukuza kipato cha kaya na mtu mmoja mmoja, chuo pia kinaendesha mafunzo ya muda mfupi na kutoa ushauri kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ufugaji nyuki juu ya namna bora ya kufanya shughuli za ufugaji nyuki.

**Dira** ya chuo ni kuwa kituo bora katika kutoa mafunzo, ushauri na kufanya tafiti za maendeleo ya ufugaji nyuki nchini na uhifadhi wa mazingira.

Chuo kimeendelea kudahili wanafunzi kwa kuzingatia taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Chuo kimeendelea kupata ongezeko kubwa la wanafunzi jinsia ya kike wanaoshiriki katika mafunzo haya. Aidha, chuo kilianza na udahili wa wanafunzi takribani 34 mwaka 2010 na kwa sasa (2022/2023) chuo kina jumla ya wanafunzi waliosajiliwa 394. Mwaka 2010 wanafunzi wa kike walikuwa ni 12 sawa na asilimia 35 na 2022 wanafunzi wa kike ni 186 sawa na asilimia 47.2. Aidha, kuanzia mwaka 2015/2016 mpaka 2021/2022 jumla ya wanafunzi 724 wamehitimu mafunzo kwa ngazi ya Astashahada na 443 wamehitimu kwa ngazi ya Stashahada.

Aidha, kwa upande wa kozi za muda mfupi na ushauri, chuo kinapokea wadau wote bila kuzingatia vigezo vya taaluma. Kuanzia mwaka 2017 mpaka 2022 chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi na kutoa ushauri kwa wadau wa sekta ya ufugaji nyuki wapatao 8,608 ambao ni pamoja na waliofika chuoni moja kwa moja na wale waliotembelewa katika maeneo yao katika ngazi za Wilaya na Mikoa.

Chuo kinaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa kujenga miundombinu mipya na kukarabati miundombinu ya zamani. Ndani ya miaka mitatu (2019 – 2022) chuo kimefanikiwa kujenga jengo la kuchakata mazao ya nyuki, ukarabati wa jengo la utawala, kununua vifaa vya kuchakata mazao ya nyuki pamoja na ujenzi wa jengo la karakana. Aidha, ndani ya kipindi hicho, chuo kimefanikiwa kuanzisha shamba darasa katika Wilaya ya Uyui mkoani Tabora katika hifadhi ya msitu wa Simbo. Hifadhi hii ipo kilometa 20 kutoka chuoni. Kuanzishwa kwa shamba hili kuna punguza gharama za kufanya mafunzo maeneo ya mbali na chuo. Msitu mwingine wa mafunzo upo Wilaya ya Sikonge na maeneo yote haya yamekuwa ni chachu ya kuendesha mafunzo kwa ufanisi.

Chuo pia kimeendelea kufanya ukarabati wa nyumba za watumishi, mifumo ya maji safi na maji taka pamoja na kuweka barabara za ndani ya eneo la chuo. Yote hayo yamekuwa yakifanyika kwa juhudi kubwa za Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na chuo chenyewe kupitia mapato yake ya ndani.


Mbali na shughuli nyingine chuo pia kinatekeleza mradi wa kuzalisha malkia wa nyuki na hivyo kuongeza makundi ya nyuki. Taarifa zinaonesha kuwa mizinga mingi ilikuwa haina makundi. Chuo kwa kuliona hilo mwaka 2020 kilianzisha mradi wa kuzalisha malkia wa nyuki ambapo hadi sasa takriban malkia 270 wameshazalishwa hivyo kuongeza makundi kwa idadi hiyo. Sehemu kubwa ya makundi yaliyoyazalishwa kwa awamu hii



*Mgeni rasmi, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka akiweka saini kitabu cha wageni baada ya kuwasili chuoni Novemba 11, 2022*

ya kwanza yametumika kwenye shamba darasa la chuo ili kuyafanyia utafiti kuona ufanisi wake hususan kama yamekuwa na tabia zile zilizokusudiwa.

Baada ya kujiridhisha na ufanisi wa makundi hayo chuo kitazalisha kwa wingi makundi ya nyuki na kuyasambaza kwa wafugaji nyuki.




| | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 | 2013/2014 | 2014/2015 | 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ME | 22 | 26 | 41 | 32 | 48 | 28 | 71 | 108 | 147 | 190 | 223 | 198 |
| KE | 12 | 12 | 19 | 19 | 31 | 21 | 52 | 92 | 119 | 163 | 185 | 176 |

*Kielelezo kinachoonesha udahili kwa jinsia kuanzia 2010/11 hadi 2021/22*



*Mgeni rasmi, Prof. Eliamani Sedoyeka (Mstari wa mbele katikati) pamoja na baadhi ya wahitimu ngazi ya Stashahada kwa mwaka 2022*

# IJUE KAMPASI YA MIZENGO PINDA YA CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

Na: Mwandishi wetu, SUA

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo - SUA kimeanzisha kampasi mpya iliyopewa jina la Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda. Kampasi hiyo ipo Kata ya Kibaoni, Halmashauri ya Mpimbwe, Wilaya ya Mlele mkoani Katavi - Nyanda za Juu Kusini. Kampasi ya Mizengo Pinda ilianzishwa mwaka 2019 kwa lengo la kupanua taaluma na kufanya tafiti mbalimbali katika nyanja za kilimo, maliasili na utalii hususani katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na maeneo jirani. Kampasi hiyo imedahili wanafunzi kwa mara ya kwanza katika mwaka wa masomo wa 2020/2021.

Kama ilivyo kwa taasisi za elimu ya juu nchini, kampasi ya Mizengo Pinda inatekeleza majukumu makuu matatu ambayo ni: kufundisha, kufanya tafiti, na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii katika nyanja za kilimo, maliasili na utalii.

Hadi sasa Kampasi ina wanafunzi wanaosoma Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki, Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao na Astashahada ya Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii. Programu hizi zimeanzishwa kimkakati na zinatolewa kwa aina ya upekee ukilinganisha na programu za aina kama hizo zinazotolewa na vyuo vingine nchini.

Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki *(Bachelor of Science in Bee Resources Management)* mbali na kufundisha ufugaji wa nyuki wa asali kama programu nyingine zilizopo hapa nchini, mafunzo ya programu hii yanaanzia kuzijua kwa undani aina zote za nyuki, mazao yake na huduma mbalimbali zitolewazo na nyuki katika mfumo wa ikolojia.

Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao *(Diploma in Crop Production and Management)* imeanzishwa ili kuendana na hali halisi ya mikoa hii ambayo ina uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo, hususani mahindi, mpunga, karanga, alizeti na ufuta. Mazao yote haya yanatumika kama mazao ya chakula na biashara. Kwa hiyo, uwepo wa programu hii katika mkoa huu unatoa fursa kwa wakulima kujifunza njia bora na za kisasa za kilimo kupitia wanataaluma wa chuo wanaotoa mafunzo ya muda mfupi pamoja na tafiti katika maeneo ya ukanda huu. Pia, wakulima wanaweza kujifunza kwa kutembelea mashamba darasa yaliyopo chuoni, ambayo hutumiwa na wanafunzi wakati wa mafunzo kwa vitendo.




*Wanafunzi wa wakipokea maelekezo wakati wa kukaribishwa chuoni*

Programu nyingi za Astashahada ya utalii nchini zimejikita zaidi kwenye kuongoza watalii na usimamizi wa hoteli za kitalii. Hata hivyo, programu ya Astashahada ya Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii *(Certificate in Tour Guiding and Hunting Operations)* imeweka msukumo mkubwa kwenye taaluma ya uwindaji wa kitalii. Jambo hilo limeifanya kuwa programu ya kipekee hapa nchini na kuvutia wadau wengi. Kwa upande mwingine chuo kipo karibu na maeneo ya utalii kama vile Hifadhi ya Taifa ya Katavi, na ya uwindaji kama vile Mapori ya Akiba ya Rukwa, Lwafi, Rungwa, na Mapori Tengefu ya Inyonga na Ugunda. Maeneo haya yanatoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo kuhusu uongozaji wa watalii na uwindaji wa kitalii.

Aidha, programu hizi zimetoa fursa kwa wataalamu kufanya tafiti mbalimbali. Mkoa wa Katavi unajulikana kwa kuwa na aina mbalimbali za nyuki na makundi mengi makubwa ya nyuki. Hali hii hutoa fursa kwa wanafunzi kuyatambua, kujua tabia na faida zake. Kwa mfano, wanafunzi wanauwezo wa kuainisha aina 30 za nyuki wanaochavusha mimea katika eneo la chuo. Kujulikana uwepo wa aina hizi za nyuki ni muhimu kwa kilimo kwa vile huchavusha mazao mengi ya kilimo hivyo kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao hayo.

Vilevile, programu hizi hutoa fursa ya kuweka mikakati bora ya uhifadhi wa mazingira, usimamizi wa rasilimali nyuki pamoja na mazao yake yote na utoaji huduma ya uhakika ya uchavushaji wa mazao ya kilimo kama vile alizeti, mahindi na ufuta. Kwa upande mwingine, uwepo wa mazao mengi ya kilimo katika maeneo ya ukanda huu unatoa fursa kwa nyuki kupata chavua na mbochi kwa ajili ya kutengeneza mazao mbalimbali ya nyuki.

Katika utalii, wanafunzi wanajifunza uwepo wa fursa za utalii zinazopatikana kwenye ufugaji nyuki kwa mfano, tiba ya nyuki na shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye mzinga. Wanafunzi pia hujifunza utalii wa kitamaduni wa makabila mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Kwa sasa Kampasi hii inaendelea na Miradi mitatu ya kiutafiti katika nyanja mbalimbali. Moja ya miradi hiyo ni ule unaolenga kutambua njia za asili zitakazosaidia kudhibiti uharibifu na upotevu wa mazao baada ya mavuno usababishwao na wadudu aina ya viwavijeshi. Mradi huu unajulikana kama *(Integrated Traditional Package for Controlling Maize weevil (Stophiluszea) to reduce post harvest losses at Katavi region).* Mradi mwingine wa kiutafiti unalenga kupata njia za kitaalamu kwa kutumia TEHAMA katika uchaguzi wa mbegu bora zenye kuhimili magonjwa. Mradi huu unajulikana kwa jina la *(Towards Breeding for Fall Armyworms resistant Maize varieties: A deep learning computer model for acceleration of the selection cycle).*

Miradi yote miwili inafadhiliwa na SUARIS kupitia mapato ya ndani ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Mradi wa tatu ni Uanzishwaji wa Kituo cha Mafunzo na Uzalishaji wa Rasilimali Nyuki katika Kampasi ya Mizengo Pinda *(Establishment of Bee Resources Training and Production Facility at Mizengo Pinda Campus).* Mradi huu umelenga kuwajengea uwezo wanafunzi na wafugaji nyuki katika kuongeza mnyororo wa thamani wa usimamizi wa rasilimali za nyuki. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF.

Tangu Kampasi ya Mizengo Pinda ilipoanzishwa mwaka 2019, imeendelea kuboresha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi na wafanyakazi kama vile kujenga na kukarabati madarasa, dahalia (*hostel*), jengo la chakula na miundombinu ya umeme na maji.



*Wanafunzi wakiwa katika shamba darasa la mazao ya kilimo*

Ili kuimarisha mafunzo kwa vitendo Kampasi imeanzisha shamba darasa la mazao ya kudumu ikiwa ni pamoja na mikorosho. Mazao mengine ya msimu kama vile mahindi na alizeti hupandwa kila mwaka. Pia, kuna shamba dogo la mafunzo eneo la kampasi ambalo husaidia mafunzo kwa vitendo yatolewayo kila siku. Shamba hilo lina mazao mbalimbali kama vile korosho, papai, embe, mahindi na mazao mengine pamoja na mbogamboga.


Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Kampasi imepanga kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Aidha, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeitengea kampasi ya Mizengo Pinda kiasi cha Dola za Kimarekani milioni nane sawa na shilingi za kitanzania bilioni 18.6 kutoka kwenye mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation - HEET) kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la mtambuka la taaluma (*multipurpose hall*), bweni la wanafunzi, jengo la chakula, kuanzisha shamba la mfano la mafunzo, kununua vifaa vya maabara, pamoja na ununuzi wa basi moja la wanafunzi.

Chuo kinawakaribisha wote wanaotaka kujiendeleza kielimu, kupata ushauri wa kitaalamu, kushirikiana kwenye utafiti katika nyanja za kilimo, maliasili na utalii.

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti: www.mizengopinda.sua.ac.tz au wasiliana nasi kupitia barua pepe principalmpc@sua.ac.tz




*Wanafunzi wakiwa katika mafunzo kwa vitendo - Hifadhi ya Taifa Katavi*



# SAFARI YANGU MAPOROMOKO YA MTO KALAMBO

*Na: Nurdin Chamuya*

Safari yangu kuja kuyaona maporomoko ya Mto Kalambo ilianzia kijijini kwetu Sangeni Wilayani Kilindi Mkoani Tanga. Habari za kuwepo kwa safari hii nilizipata kutoka kwa maafisa watatu tofauti wa Idara ya Misitu na Nyuki. Taarifa hizo zilinieleza kuwa baadhi ya wasomaji wa *Jarida* hili wamevutiwa na makala zangu za mwanzo za ***Safari yangu*** za: *Kigulu-Hakwea, Mvuleni – Rau* na ya *Mlima Hanang*'. Wasomaji hao wameshauri makala kama hizo zisikosekane kwenye kila toleo. Ili kukidhi matakwa ya wasomaji wake, wachapishaji wa *Jarida* waliamua kuandaa safari ya kwenda kwenye maporomoko ya maji ya Mto Kalambo yaliyopo katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo. Baada ya kipindi kirefu kiasi nilipigiwa simu na Bw. Petro Mholage; Afisa kutoka Idara ya Misitu na Nyuki Dodoma. "Mzee jiandae safari imeiva." Nilimjibu kwa kifupi "sawa." Hata hivyo nilimuuliza; "safari itaanzia wapi Bwana Mkubwa?" Huku akicheka alinijibu; "Dodoma Mzee." Sikutaka kujua kwa nini alicheka. Labda alilinganisha umri wake na wangu halafu mimi namwita Bwana Mkubwa.

Kwa wakati ule sikuona umuhimu wa kujua nani mfadhili wa safari hiyo. La muhimu ni kujitayarisha. Kama ningeshiriki kuandaa hii safari, nisingeshauri ianzie Dodoma. Ningependekeza ianzie Dar es Salaam. Ningeshauri tusafiri kwa treni ya TAZARA hadi Mbeya. Hii ingetoa fursa ya kuona utajiri wa rasilimali za asili zilizomo katika Hifadhi mpya ya Taifa ya Mwalimu Nyerere pamoja na Bwawa jipya la kufua umeme la Mwalimu Nyerere. Pia ningeshauri wakati wa kurudi tungetumia barabara na kufanya utalii katika Hifadhi ya Taifa Mikumi. Nilidhani kwa kufanya hivyo makala hii ingechangamka zaidi.

Bila kushurutishwa nilitii amri ya kupita Dodoma. Safari yangu ya kutoka kijijini kuja Dar es Salaam ilianza asubuhi ya Jumamosi Oktoba 29, 2022. Safari hiyo ilichukua saa sita. Njiani nilijionea kutamalaki kwa ukame mwaka huu. Hali hiyo ilinisononesha nafsi na kunijengea hofu niliwaza maisha yatakuwaje mwakani; maana kuna kila dalili za kuwepo kwa balaa la njaa. Mvua za vuli hazikunyesha kabisa. Pamoja na hali hiyo wakulima walitayarisha mashamba tayari kwa kupanda mazao pindi mvua itakaponyesha. Niliwaona wafugaji wakihangaika kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao. Nilifika Dar es Salaam na kupumzika siku ya Jumapili.

Safari ya kwenda Dodoma ilianza asubuhi ya Jumatatu Oktoba 31, 2022. Hali ya ukame haikuwa tofauti sana na ile ya Handeni – Dar es Salaam. Lile bonde la Mto Ruvu ambalo kwa kawaida kipindi hiki cha mvua za vuli ni la kijani kutokana na mashamba ya mpunga ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Ruvu na wenyeji wa vijiji na mji mdogo wa Mlandizi lilikuwa kavu kabisa. Kijani fulani kilionekana kidogo kwenye bustani ndogo ndogo za mboga mboga zilizotawanyika. Aidha, yale mashamba ya mkonge na Msitu wa Hifadhi Kitulang'halo vyote viliathiriwa na ukame havikuonesha afya! Hifadhi ya Misitu ya Mazingira

Asilia Milima Uluguru nayo kwa kiasi fulani haikupona. Miti ilipukutisha majani na chini hakukuwa na nyasi hali iliyoyanyima macho yangu uhondo wa kijani kibichi niliyoizoea. Hali ya ukame ilikuwa hivyo hivyo hadi Dodoma. Cha kushangaza sikuona mioto barabarani. Nilijiuliza imekuwaje. Jibu ni rahisi tu: kama hakuna nyasi; nini sasa cha kuchoma! Ndiyo maana mwaka huu mioto mingi inatokea kwenye misitu minene ambako kuna nyasi kavu za kutosha hivyo, chanzo chochote cha moto kikitokea basi huzusha balaa kubwa. Safari hii ilichukua takriban saa saba.

Pamoja na jiji la Dodoma kubadilika nilikumbuka mahali ilipo nyumba ya kulala wageni niliyoizoea. Nyumba hiyo ipo karibu na msikiti hii ni kwa sababu huwa sipendi kukosa Swala ya Alfajir. Niliwasiliana na wenyeji wangu na kupanga safari yetu kuelekea Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo ianze alfajir ya Jumanne Novemba mosi, 2022. Tulikubaliana kabla ya kwenda Kalambo turipoti ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa lengo la kukutana na uongozi wake kwa vile ndiyo unasimamia hifadhi hiyo.

Tulifanya mawasiliano na Mkuu wa Kanda Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Kamanda – Cosmas Ndakidemi kuhusu lengo la safari yetu na kumwomba kama kuna msaada wowote basi asisite kutupatia ili tuweze kutimiza azma yetu ya kufika kwenye maporomoko ya Mto Kalambo.

Tuliondoka kama tulivyopanga kupitia njia ya Mtera ambapo tuliliona Bwawa la kufua umeme la Mtera. Hatukuruhusiwa kupiga picha bali tulisimama na kuona maji ya Mto Ruaha Mkuu yalivyochepushwa kwa ajili ya kufua umeme. Walinzi walitushauri iwapo tungependa kupewa maelezo basi twende ofisini. Ukweli hatukuwa na muda huo, hata hivyo taarifa za mitandao zinaonesha; mbali na kufua umeme Bwawa hilo ni makazi ya mamba na viboko. Aidha, Bwawa la Mtera ni hifadhi hivyo shughuli za kibinadam haziruhusiwi kufanyika humo. Hata hivyo, nje ya Bwawa wenyeji hufanya uvuvi. Taarifa zinazidi kuonesha kuwa maji yakishafua umeme husafiri takriban kilomita 11 chini kwa chini kabla ya kurudishwa kwenye mkondo wake wa asili wa Mto Ruaha Mkuu. Baada ya kurudi mtoni maji hayo hutumika tena kufua umeme katika Bwawa la Kidatu lililopo mkoani Morogoro. Taarifa hizo zinaonesha umuhimu wa Mto Ruaha Mkuu katika ufuaji wa nishati ya umeme hapa nchini. Kwa hiyo basi, uharibifu wa mazingira ya mto huu na kuathri kiasi cha maji yake ni sawa na kujichimbia kaburi la kuzika uchumi wa nchi. Tulitoka Bwawa la Mtera na kuanza barabara yenye kona nyingi katika milima ya Nyang'oro. Tulifika Jijini Mbeya saa 12 jioni. Cha kwanza kilikuwa kuwasiliana na Kamanda Ndakidemi kumweleza kuwa tumefika na kesho saa mbili asubuhi tutakuwa wageni wake.

Ilipofika saa mbili asubuhi tuliwasili ofisini kwa Kamanda Ndakidemi. "Karibuni sana," alitukaribisha. "Asante Afande." Tuliitikia. Kamanda Ndakidemi tunafahamiana siku nyingi na mara ya mwisho tulikuwa wote Mlele kwenye mafunzo ya kijeshi. Baada ya utambulisho na kueleza lengo la safari yetu tulimwomba Kamanda Ndakidemi kutupa maelezo mafupi ya Kanda anayoiongoza akijikita zaidi katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo na Mlima Rungwe yalipo maporomoko ya maji ya Mto Kalambo na Ziwa Ngosi mtawalia.

"Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inajumuisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Rukwa. Kulingana na takwimu za NAFORMA; Kanda ina misitu yenye eneo la takriban hekta milioni 10.4. Kati ya eneo hilo la misitu; misitu ya asili ni hekta milioni 10 wakati ile ya kupandwa ni hekta laki 4. TFS katika kanda hii inasimamia misitu ya asili na misitu ya kupandwa. Kama mnavyofahamu shamba kubwa la miti nchini la Sao Hill ambalo sehemu kubwa ipo Mkoa wa Iringa lipo kwenye Kanda hii.

Mashamba mengine ni Kawetire na Kiwira yaliyopo Mkoa wa Mbeya na Mbizi lililopo Mkoa wa Rukwa. Aidha, kuna mashamba ya miti yanayomilikiwa na mashirika na watu binafsi. Kwa mantiki hiyo, kuna misitu inayosimamiwa na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Vikundi na watu binafsi. Kati ya misitu ya asili inayosimamiwa na TFS, Hifadhi za Mazingira Asilia zipo nne ambazo ni: Kalambo, Mlima Rungwe, Uzungwa na Kilombero. "Nimeelezwa kuwa mtatembelea Hifadhi za Kalambo na Mlima Rungwe" Aliuliza Kamanda Ndakidemi. "Ndiyo." Tuliitikia.

"Labda nianze na Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo," alitanabahisha Kamanda Ndakidemi na kuendelea. "Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo ipo Mkoani Rukwa Wilayani Kalambo. Hifadhi ina eneo la hekta 43,334. Aidha, Kalambo imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa viumbe hai kuanzia mimea hadi wanyama. Mbali na utajiri huo hifadhi hii ni chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Wilaya ya Kalambo. Nchi za Tanzania na Zambia hutenganishwa na maporomoko ya maji ya Mto Kalambo na bonde lake." Alinyamaza kidogo na kutuangalia kama tuna cha kuuliza.

Baada ya kimya kidogo; Kamanda Ndakidemi aliendelea kutueleza kuwa, "kivutio kikubwa cha utalii katika Hifadhi ya Kalambo ni maporomoko ya maji ya Mto Kalambo. Maporomoko ya maji ya Mto Kalambo ni ya pili kwa urefu barani Afrika; yakitanguliwa na yale ya Tugela yaliopo katika Hifadhi ya Kitaifa ya Royal Natal Kwa Zulu-Natal, Jamhuri ya Afrika Kusini. Maporomoko ya maji ya Tugela ndiyo marefu zaidi ulimwenguni. Inakadiriwa kuwa tone la maji la maporomoko ya Mto Kalambo haligusi ardhi kwa umbali wa mita 235 wakati yale ya Tugela hayagusi ardhi kwa takriban mita 411." Taarifa zinaonesha kuwa maporomoko ya maji ya Mto Kalambo ni ya 12 kwa urefu Duniani. Hata hivyo tofauti kati ya maporomoko ya maji ya Mto Kalambo na Tugela ni kuwa yale ya Kalambo ni ya kudumu wakati yale ya Tugela ni ya msimu.

Pamoja na maporomoko ya maji ndani ya Hifadhi ya Kalambo kuna sehemu yenye mapango ambamo fisi huzaliana. Aidha, msitu huu wa Miombo ni makazi ya wanyamapori kama, tembo, nguruwe pori, nyani, ngedere, ndege na mijusi wa aina mbalimbali. Pia, zipo aina mbalimbali za mimea mikubwa na midogo. Ni katika hifadhi hii zile aina tatu za miti inayopatikana kwa wingi kwenye msitu wa Miombo hupatikana japo sio kwa wingi sana na ukubwa kama ilivyokuwa hapo awali. Aina hiyo ya miti ni: Miombo, Mininga na Mitundu. Mbali na viumbe hai wanaopatikana ndani ya hifadhi, msitu huu, upo karibu sana na fukwe nzuri za Ziwa Tanganyika.

Baada ya taarifa hizo tuliondoka jijini Mbeya saa nane mchana kuelekea Wilayani Kalambo. Baada ya kufanya mawasiliano na wenyeji wetu yaani wahifadhi wa Wilaya ya Kalambo. Wahifadhi hao walishauri tulale Sumbawanga mjini na kesho yake asubuhi tukutane ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Tulikubaliana, safari ya kuelekea hifadhini ilianza asubuhi ya saa mbili baada ya kupata kifungua kinywa. Safari ilichukua kama nusu saa hivi. Tulijiunga na Wahifadhi Jackson Mchuya na Godlisen Stanley na kuanza safari ya kuelekea kwenye maporomoko ya maji ya Mto Kalambo. Njiani wahifadhi hao walitupa maelezo yaliyofanana kabisa na ya Kamanda Ndakidemi.

Tulipofika ofisi za hifadhi tulipokelewa na Mhifadhi Sadock David Nsekela, mwongoza watalii katika hifadhi hiyo. Baada ya utambulisho Mhifadhi Nsekela alianza kazi yake mara moja. “Mbali na maporomoko ya maji ya Mto Kalambo hifadhi hii inasadikika kuwa ilikuwa ni makao ya watu wa zama za ujima. Inasadikiwa kuwa takriban miaka laki moja iliyopita kuna watu waliishi katika bonde la Kalambo. Taarifa za mitandaoni zinaonesha kuwa yapo mabaki ya zana za watu hao.” Alinyamaza kidogo kuona kama tunamsikiliza na kuendelea. “Wenzetu wa Zambia wamezifanyia utafiti taarifa hizo na inasemekana wamebaini mabaki ya zana hizo za kale kama vile mashoka na vyungu. Habari zaidi zinaonesha kuwa nchi ya Zambia ipo kwenye mchakato wa kuyaingiza maporomoko ya maji ya Mto Kalambo na Bonde lake katika orodha ya UNESCO ya urithi wa Dunia.” Alitulia na kutukaribisha kwa safari ya kuteremka kwenye maporomoko.

Tulianza safari ya kuteremka kwa kutumia ngazi zilizojengwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania yaani TFS. “Kutoka hapa tulipo hadi kituo cha mwisho kilichopewa jina la Mhe. Hamisi Kigwangala ni mita 697 na kuna ngazi 1270,” alitutaarifu Mhifadhi Nsekela na kuongeza; “safari hii sio rahisi kama mnavyodhani; inataka uwe na afya ya kutosha na uvumilivu. Siwatishii ila nawandaa kisaikolojia.” Pamoja na hofu kidogo iliyoniingia nilipanga mikakati yangu kimoyomoyo. “Nuru usifuate spidi ya hawa vijana; wewe tembea polepole utafika. Jipe mapumziko ya mara kwa mara ili



*Maporomoko ya Mto Kalambo kama yanavyoonekana kituo cha Dos*

ukusanye nguvu.” Safari ikaanza. Mdogo mdogo ngazi moja baada ya nyingine. We bwana! Hata kabla ya kufika kituo cha kwanza niliyasadiki maneno ya Mhifadhi Nsekela. Safari ile haikuwa ya mchezo mchezo. Kweli ilihitaji afya na uvumilivu. Niseme tu ukweli miguu ilishaanza kutetemeka. Magoti yalikosa nguvu. Nilihisi magoti kushindwa kuzibeba hizi kilo zangu 80. “Jitahidi mzee utafika tu;” alinitia moyo Mhifadhi Nsekela. Niliitikia kwa kichwa: maana kuongea nilihisi kungenipunguzia nguvu!

Mhifadhi Nsekela alitueleza kuwa eneo tunalolikaribia linaitwa Dos Santos Silayo: Kamishna wa Uhifadhi TFS. “Katika kituo hicho cha Dos utayaona maporomoko kwa asilimia 45. Aidha, kutoka pale juu tulipoanzia safari tumetembea mita 295 na kuna ngazi 522;” alifafanua. Nilinyanyuka na kuwaomba safari iendelee. Hatimaye tulifika kituo cha Dos Santos. “Waoo!” Nilipiga kelele ya shangwe kufikia pale. Hakika taswira niliyoijenga tangu mwanzo wa safari yangu kwetu Handeni ilijidhihirisha.

Nilimshukuru Mungu kwa kufikia hatua ile. Kwa kuwa kilikuwa kipindi cha kiangazi na miti mingi ilipukutisha majani maporomoko yalionekana dhahiri shahiri.

Nilishuhudia kwa macho makavu





*Maporomoko ya Mto Kalambo kama yanavyoonekana kituo cha Mkeremi*

maporomoko yanapoanzia. Cha kushangaza ni kuwa maporomoko haya hayaonekani kama maji yanayotiririka bali mchirizi wa mvuke au ukungu mzito wenye upana wa kama mita moja na nusu hivi, unaotoka katikati ya miamba miwili na kuchirizika hadi chini kabisa na kutengeneza kishindo cha PU! Niliuliza kwa nini maji yale huonekana vile, Mhifadhi Nsekela alinieleza kuwa huo ni uthibitisho kuwa maji yale hayagusi ardhi hadi yanapofika chini. "Kile kinachoonekana kama ukungu mzito kinatokana na maji kupingwa na upepo." Alifafanua na kuongeza. "Ukiwa hapa (Kituo cha Dos) huyaoni maporomoko yanapoishia bali unayaona vizuri zaidi pale yanapoanzia."

"Mzee naiona furaha yako baada ya kufika hapo. Nadhani hutayaamini macho yako utakapofika vituo vya Afande Mbaraka Mkeremi na kile cha Mhe. Hamisi Kigwangala ambapo utayaona maporomoko kwa asilimia 75 na 98 mtawalia." Mhifadhi Nsekela alishindwa kuficha hisia zake juu yangu. Baada ya kauli yake hiyo; tuliendelea na safari. Hata hivyo, jinsi tulivyokuwa tunazidi kushuka nilihisi mwili kukosa nguvu. Nilidhani ni sababu ya utu uzima. Nilimwangalia Mhifadhi Nsekela na macho yetu yalipogongana alinishauri: "Mzee ukijisikia kuchoka pumzika! Usijilazimishe kwa vile hewa inapungua jinsi tunavyozidi kwenda chini." Nilifuata maagizo yake na hatimae nilifika kituo cha Afande Mkeremi. Hapo niliyaona maporomoko kwa asilimia 75 kama alivyoeleza Mhifadhi Nsekela pale kituo cha Dos. Kwa kweli mtu akifika kwenye hivi vituo husahau machungu yote aliyopitia kabla. Ule mchirizi wa mvuke mzito unaonekana karibu mara mbili zaidi ya ilivyokuwa pale kituo cha Profesa Dos. "Kituo hiki kimepewa jina la Mwenyekiti wa Bodi ya TFS Afande Mbaraka Mkeremi. Kwa kukienzi kituo hiki; Afande Mkeremi ameweka rekodi ya kupandisha hadi kule juu inakoanzia safari kwa kukimbia bila kusimama popote. Hadi leo hii hakuna aliyejaribu kufanya hivyo." Alitueleza Mhifadhi Nsekela. Nilikiangalia kile kipande cha kupandisha juu na kujisemesha kimoyomoyo "Nuru wakati wa kurudi usijaribu; utapasua moyo na ndiyo itakuwa mwisho wako!" Tafakuri yangu ilikatishwa na sauti ya utani wa dhahiri ya Bw. Mholage; afisa tuliyefuatana kutoka Idara ya Misitu na Nyuki Dodoma aliposema. "Nadhani leo mzee atataka kuvunja rekodi ya afande wake kwani naona jinsi alivyojipanga kukimbia bila kusimama kutoka kituo cha Mhe. Kigwangala hapo chini hadi juu!" Alisema huku akitabasamu kuashiria dhahiri utani wake. Nilimwangalia tu wala sikumjibu kwa vile nilijua kama angelifahamu ninayowaza wala asingeleta utani ule. "Kutoka mwanzo wa safari hadi kituo hiki cha Afande Mkeremi tumetembea mita 522 ambazo zina ngazi 953." Alitueleza Mhifadhi Nsekela.

"Haya safari iendelee." Alitoa amri Mhifadhi Nsekela. Safari ikaanza tena kuelekea kituo cha Mhe. Kigwangala. Tulishuka polepole ngazi kwa ngazi. Kama kawaida: nikichoka navuta pumzi. Hatimaye tulifika kituo cha Kigwangala. Hapo niliyaona maporomoko kwa uzuri zaidi. Chini kabisa maji yanaonekana kutengeneza bwawa. Bwawa ambalo lilionekana kama chungu na maji yake yanarukaruka kama vile yanayochemka. *Mchemko* ule wa maji ulinakshiwa na rangi za upinde wa mvua. Hii ni kutokana na kupigwa na miale ya jua. Hakika kwangu niliona kuwa maporomoko yale ni ushuhuda tosha wa ***Ukuu wa Uumbaji wa Mwenyezi Mungu***. Nilimshukuru Mungu kwa kunifikisha pale na kujionea maajabu yake kwani niliamini si kwa uwezo wangu bali ni kwa Rehema Zake. Safari ya kutoka juu hadi kituo cha Kigwangala ilituchukua takribani saa moja.



*Maporomoko ya Mto Kalambo kama yanavyoonekana kituo cha Mhe. Kigwangalla*

Kiongozi wetu Mhifadhi Nsekela alishauri tuishie hapo kwani kwenda chini ngazi bado hazijajengwa, hivyo kushuka na kupandisha kungechukua muda mrefu. Tulimshukuru na kumweleza kuwa tulichokifuata hakika tumekipata. Safari ya kupandisha ilianza baada ya kupumzika kidogo. Kama kawaida yangu; nilipandisha polepole na kujipa mapumziko ya mara kwa mara. Kilichonishangaza katika safari hii ya kupandisha ambayo kwa kweli niliihofia sana ni kuwa jinsi tunavyozidi kupanda hewa iliongezeka na hivyo kuwa na nguvu zaidi ukilinganisha na wakati wa kushuka. Tulipofika kituo cha Dos nilipigwa na upepo mwanana kiasi kwamba nilisema nitafika pale juu muda si mrefu. Na kweli nikakamilisha safari ya kujionea maporomoko ya Mto Kalambo salama salmin baada ya safari ya saa nne.

"Wageni wangu nadhani kabla miili haijapoa twendeni mkaone pale maporomoko yanapoanzia;" alishauri Mhifadhi Nsekela. Safari ilianza tena. Safari hii ya kama



*Chanzo cha Maporomoko ya Mto Kalambo*

kilomita moja na nusu haikuwa ngumu kama ya kushuka au kupandisha kwenda au kutoka kwenye maporomoko. Tulifika sehemu ambayo maporomoko huanzia. Hapo Mto Kalambo hutengeneza bwawa dogo kabla ya maji yake kutiririka katikati ya miamba miwili. Nilitamani kuogelea kwenye bwawa lile. Lakini nilijenga hofu hivyo; nilinawa uso na kichwa kwa lengo la kuondoa uchovu.

“He: Mzee unachota baraka siyo? Maji ya sehemu hii yanaaminiwa na wenyeji kuwa yana baraka! Alieleza Mhifadhi Nsekela. “Wala sikulijua hilo Bwana Mdogo!” Nilimjibu kwa mkato na kuendelea na zoezi langu la kunawa. Watson aliniunga mkono sijui lengo lake lilikuwa kama langu au la.

Baada ya zoezi la kunawa uso, kichwa na mikono tulirudi hadi palepale tulipoanzia safari na kuanza safari nyingine kuelekea *view point* ambapo Ziwa Tanganyika linaonekana. Tulipofika *view point* mbali na kuliona Ziwa Tanganyika tuliona uwanda mpana ulihanikizwa na Bonde kubwa lenye mwanguko mkali pamoja na vilima na mabonde madogo madogo, Bandari ya Kasanga, miji na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Mandhari hayo huyapa mazingira ya eneo la hifadhi kuwa na mvuto wa aina yake machoni.

Humu ndani kuna mito, vijito na ardhioevu za kudumu na za muda. Aidha, kuna vilima na mabonde madogo madogo.” Alitueleza Mhifadhi Nsekela.

Aidha, taarifa zinaonesha kuwa ndani ya hifadhi hii kuna mito mingine ya kudumu mbali na Kalambo. Achilia mbali mito ya muda. Mito yote hii hutiririsha maji Ziwa Tanganyika. Vilevile karibu ya hifadhi hii kuna kijito chenye maji moto kilichopo kijiji cha Kizombwe. Mbali na vivutio hivyo, mtalii pia anaweza kufurahia na kucheza ngoma za makabila ya Wafipa na Warungu katika vijiji vya Kalembo, Kisumba na Kasote.

“Tahadhari kubwa humu ndani ya hifadhi ni kuwa kuna nyoka wa aina mbalimbali na wengine wana rangi za kuvutia sana!” alieleza Mhifadhi Nsekela na kuonya. “Msipendelee kushikashika miti kwani nyoka wengi hufanana na mazingira na hupenda kujificha kwenye miti.”

“Wageni wengi hufika Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo kwa ajili ya kuweka kambi za kitalii au utafiti na mafunzo, kuburudisha nafsi (*picnicking*), kutembea, kupiga picha za video na mnato, kuogelea, kuangalia ndege na wanyamapori, kutuliza mawazo na kutafakari mambo mazito na hata kuona maumbile ya nchi.

Hifadhi hii inafikika kwa barabara kutoka Mjini Mbeya kupitia Tunduma, Sumbawanga, Matai hadi ofisi za hifadhi. Hata hivyo, mtalii anaweza kuja kwa ndege hadi Uwanja wa ndege Songwe ulioko Mbeya ama akatua viwanja vya ndege vya Sumbawanga au Mpanda na baadaye kusafiri kwa barabara hadi hifadhini. Vile vile mtalii anaweza kufika Hifadhi ya Kalambo kutoka Dar es Salaam kwa treni ya TAZARA hadi mji mdogo wa Tunduma na kusafiri kwa barabara mpaka Sumbawanga hadi hifadhini.

Mtalii aliyepanga kutembelea hifadhi ya Kalambo anaweza pia kutembelea fukwe za maziwa Tanganyika na Nyasa, Hifadhi za Taifa za Katavi, Kitulo na Ruaha. Vilevile, anaweza kutembelea Kimondo kilichopo karibu na mji wa Mbozi Mkoani Songwe; Kijungu na Daraja la Mungu vilivyopo Wilayani Rungwe Mkoa wa Mbeya. Mbali na vivutio hivyo; mtalii anaweza kutembelea Hifadhi za Mazingira Asilia za Mlima Rungwe, Uzungwa, Kilombero, Mashamba ya miti Sao Hill, Kawetire, Kiwira na Mbizi.

Mgeni yeyote anaweza kupata huduma za malazi, chakula na viburudisho katika miji ya Sumbawanga, Namanyere na Matai. Ndani ya hifadhi zinapatikana huduma za kambi za mahema katika maeneo ya Wangabo, Ndakidemi na Hon. Tano Mwera. Uongozi wa TFS unawakaribisha wawekezaji kuwekeza katika kutoa huduma mbalimbali za malazi, chakula na viburudisho kama vile hoteli na migahawa.

Safari ya kutoka hifadhini Kalambo kurudi Mbeya ilianza saa 10 jioni kupitia Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo yaani mji wa Matai, Manispaa ya Sumbangwa, mji mdogo wa Tunduma hadi Jijini Mbeya. Tulifika Jijini Mbeya saa sita na nusu usiku.



***Safari ya maporomoko ya maji ya Mto Kalambo ni safari isiyoisha hamu: na hakika inaburudisha akili, nafsi na kutoa msongo wa mawazo.***